Kikao cha Tano – Tarehe 17 Oktoba, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 29

Kudumishwa Majina ya Asili ya Mitaa ya Zanzibar na Mashujaa Wake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu nambari 29, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa uteuzi alioupata hivi majuzi na hii inatokana na umakini wake na uimara wake na hata wananchi wa Jimbo la Tumbatu nadhani hawajafanya kosa kumchagua kwa vipindi vitatu mfululizo na tunategemea na kwa kipindi cha nne Mwenyezi Mungu akipenda. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, swali langu nambari 29 anijibu, ni hayo tu.

Zanzibar ni nchi ambayo mitaa yake ina majina mazuri ya asili na mingi yao inatokana na simulizi nzuri za historia ya kuitwa kwake, mfano wa mitaa hiyo ni Miti Ulaya, Mfereji Maringo, Misufini, Mfenesi Mazizi n.k.

Na kwa kuwa majina ya mitaa hiyo ya asili imeanza kutoweka taratibu na alama zake mfano Mfereji wa Wima na badala yake sasa mitaa hiyo kubadilisha majina na kuitwa majina ya kigeni kama Michenzani – nyuma ya Mwembe Kisonge kuitwa Alabama, Mfereji wa Wima kuitwa Ajax n.k sambamba na majina ya shule na barabara ambazo majina yake hayaakisi historia yetu na ya watu wetu watukufu wa Zanzibar ambao baadhi yao na bado mpaka leo hawajaenziwa na badala yake tunawaenzi watu wengine nje ya Zanzibar.

(a) Je kwanini mamlaka zinazohusika haziweki mabango maalum njiani yenye majina ya mitaa hiyo ili kuienzi na kudumisha asili ya majina ya mitaa hiyo?
(b) Wizara haioni kuacha majina ya asili ya mitaa yetu itoweke na kupoteza asili ya utamaduni wetu ni kusalimu amri kwa athari za utandawazi zinazolazimisha wigo wa tamaduni za kigeni?

(c) Kwa nini majina ya majengo ya shule na barabara za Zanzibar mengi hayatokani na majina ya mashujaa wa asili ya Zanzibar na badala yake kuitwa majina ya watu wa nje ya Zanzibar kama vile skuli ya Haile Sellassie, BenBella, Nkurumah n.k barabara ya Kaunda n.k.?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba nifanye masahihisho ya kuchaguliwa kwangu na wananchi wa Jimbo la Tumbatu. Yeye alisema nimechaguliwa katika vipindi vitatu mfululizo. Nimeshachaguliwa katika vipindi vinne mfululizo.

Mhe. Spika, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kazi ya uwekaji wa mabango maalumu yenye majina ya mitaa imekua ikiendelea kupitia mradi wa **ANWANI NA MAKAAZI CHINI YA SHIRIKA LA POSTA,** unaozishirikisha taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa kuanzia kazi hiyo inafanyika kwa majaribio katika maeneo ya Chukwani na Mombasa yaliomo katika Wilaya ya Magharibi Unguja na Limbani na Selemu yaliomo Wilaya ya Wete Pemba. Lengo ni kuifanya kazi ya kuweka majina ya mitaa na njia kwa Zanzíbar nzima.

(b) Serikali inatambua hilo na ndio maana katika utayarishaji wa majina ya maeneo inawashirikisha ipasavyo viongozi na wananchi wa maeneo hayo wenye rika mbali mbali.

(c) Majina ya skuli kama Haile Sellassie, BenBella, Nkurumah barabara ya Kaunda zina historia muhimu kwa Zanzíbar na kwa Afrika kwa ujumla. Ni vyema tukaendeleza kuitunza historia hizo. Kwa wale washujaa wa asili ya Zanzíbar tayari maeneo mbali mbali yamekuwa yakipewa majina yao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

a) Je, viongozi wetu wa kitaifa waliopita na waliokuwemo, watazingatiwa vipi majina yao ukizingatia Rais wetu Marehemu Dk. Idrissa Abdulwakili,

Sheikh Abdu Jumbe, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Maalim Seif Sharif Hamad na wengi wengineo ili kuweka majina hayo?

b) Mhe. Spika, kwa nini majina hayo hivi sasa hayapigwi marufuku kama majina ya Mfereji wa Wima kuitwa Ages au Alabama, kwa kuzingatia majina hayo kupoteza hadhi ya majina matukufu ya Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

a) Mhe. Spika, kwanza nataka nimthibitishie kwamba katika mradi huu ambao unafanywa chini ya Shirika la Posta na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, tutazingatia majina ya waasisi wote wakiwemo waasisi wa Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, pamoja na viongozi mbali mbali ambao wameitumikia nchi hii kwa uzalendo mkubwa sana.

b) Kwa nini majina mengine hayapigwi marufuku, akatoa mfano jina la Mfereji wa Wima. Jina la Mfereji wa Wima ni jina la eneo lile la Mfereji wa Wima kutokana na *nature* yake kuwepo ule mfereji wa wima, sio jina la barabara.

Lakini jengine jina la Alabama sio jina la asilini ni jina la maskani, kwa hivyo jina la maskani haliwezi kuhesabiwa kama ni jina la mtaa, lakini kwa sababu ya pale maskani ilipo ndio maana watu wanauita ule mtaa ni jina la Alabama. Sasa katika mapitio ya majina ya mitaa wizara yangu itahakikisha inayapitia majina ya mitaa yote, ile ambayo tunahisi bado iendelee.

Kwa mfano, yale majina ambayo yameelezwa ya kina Ahmed Benbella, Nkrumah, Kaunda. Kama tujuavyo nchi hii tulifanya mapinduzi mwaka 1964 na katika kufanya mapinduzi hayo tulishirikiana na waliokuwa viongozi wa ukombozi katika nchi nyingi za Afrika. Sasa katika hali hiyo bado tunatambua mchango wao kwa Zanzibar katika kuikomboa Zanzibar, lakini yale majina kwa mfano kama Alabama tutayapitia upya, kwa sababu sio majina hasa rasmi ni majina ambayo yalianzishwa na maskani.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, asubuhi ya leo kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili la kuweka mitaa na kugawa majina na kuweka maeneo wazi, ni sehemu ambayo ni muhimu sana kwa sababu inarahisisha hata mgeni ikiwa anataka kwenda sehemu ambayo haijui inakuwa ni rahisi kuijua na ikiwa kuna mzingo mtu anataka kuletewa basi unakuja moja kwa moja mpaka kwenye mtaa wake.

Mhe. Spika, wakati nilipokuwa kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, tulipata fursa ya kutembelea Dodoma katika maeneo hayo ambayo kuwa yamewekwa majina ya asili na mitaa kugawa maeneo. Lakini kule niliwaona wenzetu tayari wana mafanikio makubwa na tayari wameshaweka vibao baina ya barabara na barabara na mitaa.

Mhe. Spika: Haya uliza swali.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Lakini hapa kwetu kwa sababu Mhe. Waziri amesema kwamba kuna majaribio na ametaja maeneo, lakini mpaka sasa hivi hatuoni kuwekwa hizo alama. Je, ni lini hasa zitaanza kuwekwa hizo alama ili watu wapate urahisi wa kuyajua hayo maeneo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu mama kwamba hivi sasa tuna mradi chini ya ufadhili wa Shirika la Posta tunaufanya kwa Unguja na Pemba, kwa madhumuni ya kutambua mitaa iliopo hivi sasa. Miji hii yote sasa hivi hasa Mji wa Zanzibar tuko katika mpango mkuu wa *master plan* ya mji. Hapo itakapokuwa imekamilika na haya majaribio ambayo tunayafanya chini ya posta na sisi wenyewe kwa kuzingatia mahitaji kama nilivyosema mwanzo kuzingatia waasisi mbali mbali na viongozi mashuhuri wa nchi yetu, basi wakati huo kutakuwa na ramani ya mji na ramani ya nchi. Hiyo ndio itakayoongoza sambamba na hayo majina ambayo yatakuwa yamewekwa ma mamlaka zinazohusika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba majina ya mikoa na wilaya ni majina yanayoainisha mipaka, yaani Kaskazini A, Kaskazini B, Magharibi, Mashariki. Je, haiko haja ya kubadilisha majina haya katika mkoa na wilaya ili kuangalia matukio muhimu ambayo yamefanyika katika wilaya ile ambayo tutaibadilisha jina na wilaya ile ikaendana na yale matukio muhimu?

Kwa mfano, Wilaya ya Mjini kwa sababu kuna historia ya utalii, ina maana litafutwe jina ambalo ni *common* la pale kuliko kuweka majina haya ya mipaka ambapo Kaskazini A na Kaskazini B ni majina ambayo yanaainisha mipaka, kwa nini usilifikirie suala hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe ameshauri kutokana na majina yalivyo sasa hivi ya wilaya na mikoa na akatolea mfano wa Wilaya ya Mjini au Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B.

Mhe. Spika, nataka nimueleze kwamba jukumu hili la kugawa maeneo liko chini ya utaratibu maalumu ambao unazingatiwa kwa mujibu wa sheria. Sasa wakati huo itakapofika haja ya kufanya hivyo, sio tatizo kufanya hivyo, lakini ni lazima lifanywe kwa mujibu wa taratibu ziliopo. Ahsante sana.

Nam. 60

Vipaombele Katika Ujenzi wa Barabara

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa mfuko wa barabara ni mfuko wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unaofanya kazi zake kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii bila kujali itikadi au jiografia mlipa kodi huyu alipo. Na kwa kuwa dhamira kubwa za mfuko huu ni kuzitunza barabara zote za Unguja na Pemba.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kufanya matengenezo ya barabara kilomita 285.762 zote hizo zikiwa za Unguja kwa mwaka 2012/2013 na hatimae kuweka malengo ya kujenga kilomita 285.762 bila kuingiza barabara hata moja ya Pemba kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika Baraza lako Tukufu katika Bajeti yake ya 2013/2014?

Mhe. Waziri wa Fedha - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 60 lenye vifungu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Mfuko wa Barabara ni mfuko wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na lengo lake kuu ni kuzifanyia matengenezo barabara za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Mfuko wa Barabara ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 5,551,000,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Katika kutekeleza majukumu hayo, fedha hizo zilipangwa kutumika kwa mpango ufuatao.

Kwanza shilingi bilioni 2,958,143,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Unguja, na shilingi bilioni 1,642,436,900.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Pemba na shilingi milioni 950,420.100 kwa ajili ya matengenezo ya dharura, mitambo na zana pamoja na kuchangia miradi ya barabara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa matengenezo ya barabara katika visiwa vya Unguja na Pemba, mwaka wa fedha 2012/13, Mfuko wa Barabara umezifanyia matengenezo barabara za Pemba zifuatazo:-

1. Matengenezo ya barabara ya Machomane - Meli tano
2. Matengenezo ya barabara ya Chake - Wesha
3. Matengenezo ya barabara ya Wesha - Mkumbuu
4. Matengenezo ya barabara ya Finya - Kicha
5. Ujenzi wa Madaraja ya Mkia wa Ng'ombe na Shangafu
6. Ujenzi wa Kalvati barabara ya Finya - Kicha
7. Ujenzi wa kalvati barabara ya Kilindi
8. Ujenzi wa Kalvati barabara ya Chake - Mkoani eneo la Mtambile na
9. Ujenzi wa mitaro ya Masota na Mkoani

Mhe. Spika, kazi nyengine zilizofanywa kwa upande wa Pemba ni moja na kuzifanyia usafi na uzibaji wa viraka kwa barabara ya Ole – Mzambarauni na Chake Chake –Mkoani, pamoja na kupeleka umeme Kware ya Vitongoji na utengenezaji wa zana mbali mbali za ujenzi wa barabara.

Mhe. Spika, napenda pia ifahamike kuwa Mfuko wa Barabara kufanya kazi zake kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano ya kazi baina ya mfuko na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano yaani *Performance Agreement* kwa kila mwaka. Katika makubaliano hayo kuainisha kazi zitakazofanywa kwa mwaka husika pamoja na gharama zake.

Mhe. Spika, kwa maelezo hayo, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kuwa Mfuko wa Barabara katika mwaka wa fedha 2012/2013 umefanya kazi zake katika kisiwa cha Pemba na utaendelea kufanya hivyo kwa Zanzibar nzima.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa hapa Mhe. Waziri wa Fedha, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hili nadhani atakubaliana na mimi kwamba katika takwimu tulizopewa katika kitabu cha bajeti mara hii zilikuwa na makosa au ni *printing mistake* tu. Kwa sababu zile takwimu zilionesha tu barabara zilizoshughulikiwa ni za Unguja tu. Kwa hivyo, je hiyo imekosewa kwa *printing mistake* au ni mambo mengine?

b) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba Pemba wamepewa karibu shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Pemba. Je, ni sababu gani za msingi alizoziona Mhe. Waziri kwamba barabara muhimu za ndani, kama inayotoka Vikunguni kupitia Ng'ambwa hadi Gombani Mpya ambapo hii ni barabara muhimu sana, sio kwa Pemba tu, lakini hata hapa Unguja, kwa sababu ndizi zinazotoka kule zinauzwa mpaka katika soko la hapa Unguja Darajani?

Vile vile, barabara muhimu ambayo hata Mhe. Rais aliahidi kuitengeneza kwa kiwango cha lami ile ya kutoka Vikunguni mpaka Scaling Mesi pale mjengo wa banda. Kwa nini zisitumike hizi pesa nazo kwa kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais, zisitumike hizi shilingi milioni 1.6, kutekeleza ahadi aliyoitoa Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Aman Abeid Aman Karume kwa kuweka kiwango cha lami barabara muhimu ile ya Vikunguni hadi kufikia Scaling Mes, ni sababu gani za msingi?

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza nilipoona zile takwimu sikujua amezipata wapi, kwa sababu katika swali lake la msingi hakunieleza kwamba zilikuwa ziko katika kitabu cha bajeti au zimetoka wapi. Lakini ninamuahidi kuwa nitajaribu kuzifuatilia zile takwimu angalau niweze kujua kwamba kama zimekosewa au tafsiri yake ni tofauti na zilivyo, halafu baadae nitamuarifu kwa maandishi.

Suala la pili Mhe. Spika, ni lazima ikumbukwe kwamba Mfuko wa Barabara kazi yake kubwa ni kukarabati barabara sio kujenga barabara. Lakini kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, kama serikali itaomba Mfuko wa Barabara kujenga barabara ambazo sio ndefu sana, Mfuko wa Barabara una uwezo wa kuchangia katika ujenzi wa barabara hizo.

Mhe. Spika, nilieleza *Performance Agreement* baina ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano watakapokubaliana na mfuko kwamba mwaka huu tunataka barabara hii tusaidiwe kujengwa, basi vile vile zitajengwa. Hizo barabara alizozieleza Mhe. Mwakilishi, nakubaliana naye kwamba ni muhimu. Mimi nadhani hili suala nitalichukua na nitashauriana na mfuko kwa kushirikiana na

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano waweze kuzisaidia kuzijenga, kama itakidhi vile vijengo vya kujengwa na mfuko.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, katika mchakato wa ukarabati wa barabara ya Mkoani, zile sehemu ambazo zinakusudiwa kufanyiwa ukarabati zimekatwa ni muda mrefu sasa.

a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea mpaka leo kuwa sehemu zile hazijalipwa na hatimaye wananchi wanakula vumbi sana?

b) Je, serikali inajipanga vipi kuwalipa fidia wananchi wale walioathirika kwa kubugia vumbi muda mrefu?

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza barabara inapokatwa inategemea nani aliyeikata ile barabara na kutokana na makubaliano baina ya Idara ya Barabara na idara zinazokata zile barabara, ni lazima barabara zile zinatakiwa kufidia matengenezo ya zile barabara. Hasa mkataji mkubwa wa barabara ni Idara ya Maji. Kwa hivyo, inawezekana kwamba bado hawajafidiwa, lakini ukweli ni kwamba hizi barabara zinapaswa kuzibwa ili zirejeshwe katika hadhi yake. Kwa sababu sijajua ni nani aliyeikata ile barabara na Mhe. Mwakilishi hakusema ni nani aliyekata ile barabara.

Kwa hivyo, suala la msingi ni kutafuta ni nani aliyekata ile barabara na kwa utaratibu upi, kama ni Idara ya Maji, basi ni kufidia ili ile barabara iweze kurejeshwa katika hali yake ya kawaida. Mhe. Spika, nitakachokifanya ni kufanya mawasiliano na wenzangu ili tuweze kuona kwamba ni nani ambao wameikata na kwa utaratibu upi ili iweze kurudiwa.

Mhe. Spika, suala la fidia la vumbi. Suala hili haliko katika utaratibu wa kisheria. Nadhani wananchi wanatakiwa wakae mbali tu ya mavumbi, ili kuepukana na dhara ya afya zao.

Mhe. Rufai Said Rufai: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, katika jibu mama Mhe. Waziri alisema kwamba Mfuko wa Barabara katika barabara ilizotengeneza ni moja ni ya Ole - Konde. Lakini Mhe. Spika, barabara hii ya Ole - Konde kutokana na matengenezo ya barabara nyengine za H Yong, barabara hii imechafuka sana.

Naomba kumuuliza Mhe. Waziri, Je uharibifu huu unaoendelea wa barabara ile iko katika mikono ya nani matengenezo mapya?

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, ni kweli. Wakati tunapojenga baadhi ya barabara kuna baadhi ya barabara zinaharibika hasa kutokana na kupitisha vile vifaa vizito na kwa sababu zile shughuli zinazofanywa ni shughuli zetu sisi serikali, ni dhahiri kwamba baadae mfuko huu utalazimika tena kuitengeneza ile barabara. Kwa hivyo, namuomba tu Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi. Sasa hivi kama bado wanaendelea kupeleka vifaa vizito huwezi ukaikarabati sasa hivi, lakini watakapomaliza tu basi itabidi na hii barabara nayo ifanyiwe ukarabati.

Nam. 61

Mfuko wa Barabara na Miradi Mipya

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa mfuko wa Barabara uliundwa ili kusimamia matengenezo ya barabara nchini na kwa kuwa mfuko huu hauna vyanzo vya kutosha vya mapato kwani hutegemea zaidi kodi itokanayo na mafuta pekee.

(a) Je, ni lini Mfuko huu utapima vyanzo vikuu vya mapato ya Serikali?

(b) Ni kwa kiasi gani Mfuko wa barabara hushirikishwa katika kubuni miradi mipya ya Serikali?

Mhe. Waziri wa Fedha - Alijibu:-

Mhe. Spika, Kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 61 lenye vifungu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Barabara nambari 2 ya mwaka 2001, pamoja na marekebisho yake yaliyofanywa mwaka 2008. Vyanzo vikuu vya mapato ya mfuko vilivyotajwa kwa mujibu wa sheria ni kodi ya mafuta yaani (*petrol na dieseal*), ambayo kwa sasa hutozwa TShs. 100 kwa lita.

   Aidha, kwa mujibu wa sheria hiyo, mfuko unaweza kumuomba Mhe. Waziri wenye dhamana ya fedha mapato mengine au kuanzisha vianzo vyengine kwa ajili ya mfuko.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa uongozi wa mfuko unafanya utafiti ili kuweza kufahamu mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara zetu kulingana na uwezo wetu wa kuzifanyia matengenezo. Utafiti huo utasaidia kuona kuwa kama mfuko upatiwe fedha za ziada kutoka serikalini, au kuanzishwa vyanzo vyengine vya mapato ya mfuko.

b) Mhe. Spika, jukumu la mfuko kwa mujibu wa sheria ya mfuko ni kukarabati barabara na sio kubuni au kushiriki katika kubuni miradi mipya ya serikali. Ubunifu wa miradi mipya ya serikali ni jukumu la Tume ya Mipango kwa kushirikiana na uongozi wa sekta ya barabara. Kwa mgawanyo huo wa majukumu, Mfuko wa Barabara haushiriki katika kubuni miradi mpya ya serikali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba fedha za Mfuko wa Barabara ni kwa ajili ya kukarabati barabara na sio kujenga barabara.

Kwa kuwa miradi mingi sasa hivi ipo na makampuni mengi yamepewa kazi ya kujenga barabara mpya, sambamba na kuchafuka kwa barabara kongwe ziliopo. Je, kwa mnasaba huo Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuletwa sheria hapa Barazani ili kuweza kuupatia mfuko huu vyanzo vya ziada, ikiwa ni pamoja na kutoa asilimia 10 ya mapato wanayopewa wakandarasi wa barabara mara baada ya kumaliza *project* zao, watowe asilimia 10 na kuileta katika mfuko huu, ili kukarabati hizi barabara ambazo wanaziharibu sana wale jamaa wa H. Yang na makampuni mengine.

Mhe.Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, hoja ya wakandorasi ya kutokuziharibu barabara zilizojengwa ni ya msingi kabisa, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kabisa. Wakandorasi ni lazima wasiziharibu barabara zililizojengwa, wakati wao wanapotaka kujenga barabara nyengine.

Lakini inatokea barabara hizi kuharibika kwa sababu ya kupitisha vyombo vyao. Wakati mwengine inatokea barabara hizi kuharibika kwa sababu ya kuhamisha barabara zao. Je, tufanye nini, wazo alilolitoa mimi nakubaliana nalo Mhe. Mwakilishi na ninamuomba Mhe. Mwakilishi wazo lake aliandike kwa kirefu atuletee halafu na sisi tuweze kulifanyia kazi pale wizarani. Kama kutengeneza sheria mpya au kuifanyia marekebisho sheria yetu ya mfuko, ili iweze kuwa na chanzo cha ziada katika kukarabati barabara zetu, nakubaliana naye kabisa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, ahsante nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu ya swali mama alivyoelezea kwamba lengo na dhamira ya Mfuko wa Barabara ni kufanya matengenezo au marekebisho ya zile barabara ambazo zimeathirika.

Kwa hivyo, mimi nataka kujua tu labda vigezo wanavyotumia vya matengenezo ya hizo barabara, kwa sababu tunazo barabara ambazo zina muda mrefu na hazipitiki lakini hatujaona huu Mfuko wa barabara kutengewa mafao kwa ajili ya kuzitengeneza barabara zile. Kwa mfano, tunayo barabara ya Biziredi – Mlandege, barabara ya Mitiulaya – Kinazini pia kuna barabara ya Mlandege – Gulioni. Sasa hapa ninataka kujua tu utaratibu wanaotumia katika kufanya haya ya barabara.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza katika swali Nam. 60 kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Mfuko wa Barabara wanakaa na kupanga ni barabara gani safari hii ziweze kufanyiwa ukarabati. Kwa muono wangu barabara ambazo zitakazokuwa zimeharibika sana ningependa zianze kufanyiwa ukarabati mwanzo na nyengine ziweze kufuata baadaye. Lakini kuna uwezekano kwamba wanafanya hivi kwa sababu ya *distribution* ya fedha, ili ziweze kufanya matengenezo katika mikoa karibu yote japo kwa barabara moja baada ya moja.

Sasa hizi barabara ambazo Mhe. Mwakilishi amezizungumza na mimi nimezipitia barabara hizi kwa kipindi kirefu sana nadhani ni vyema tutawasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika ile *performance agreement* yao katika kipindi kijacho na barabara hizi basi waweze kuziweka kwenye malengo yao, ili waweze kuzifanyia ukarabati.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wakati sheria ilipopitishwa iliweka kwamba kwa kila lita moja itolewe shilingi 100 katika kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Kwa kuwa thamani ya shilingi 100 kwa wakati ule ni tofauti na thamani ya shilingi 100 ya sasa hali ambayo inapelekea kwa kweli kuwa na pengo kubwa la nakisi baina ya bajeti ya kipindi kile na cha sasa.

(a) Je, serikali imeweka utaratibu gani wa ku-subsidies hili pengo la gharama baina ya wakati ule na wa sasa?

(b) Kwa kuwa serikali imeruhusu kutolewa msamaha fulani kwa makampuni haya katika kodi zao za mafuta. Vile vile imedhihirika kwamba hivi sasa makampuni hutumia ujanja wa kuchukua mafuta kwa wingi na kuuza kwa njia za magendo kitu kinachopelekea wizi mkubwa sana wa kodi ya serikali kupitia mafuta. Hivi serikali inalifahamu hilo na kama inalifahamu imejiandaa vipi kulitatua tatizo hilo?

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza ninakubaliana naye kwamba tokea tumeitunga hii sheria tumeweka ile shilingi 100 kwenye nyongeza ya mafuta kama ndio yende katika masuala mazima ya kukarabati barabara zetu. Mtandao wa barabara umeongezeka na umekuwa mkubwa zaidi, lakini thamani ya shilingi imepungua.

Kwa hivyo, mimi nataka nimuombe Mhe. Omar Ali Shehe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia kwako Mhe. Spika, katika bajeti ijao basi tufikirie angalau kuongeza japo shilingi 50 kwa ajili ya kuzipeleka kwenye Mfuko wa Barabara. Kwa kweli hali hiyo, itatusaidia zaidi kuongeza mapato ya Mfuko wa Barabara lakini itatusaidia zaidi kuongeza thamani ya ile shilingi 100. Kwa maana hiyo, namuomba tungefanya hivi ingeweza kutusaidia zaidi.

Pili, alizungumzia kuhusu suala la wizi wa kodi kupitia kwenye mafuta. Mhe. Spika, hivi sasa tunajitahidi sana kuyaangalia makampuni yote ambayo yanaingiza mafuta pamoja na yanayopata kodi kupitia kwenye mafuta au yanayopata *exemption* kupitia kwenye mafuta, kwa kweli tunajitahidi sana kudhibiti, ili haya yaweze kuondoka. Kwa hivyo, ninamuhakikishia kwamba katika kipindi kifupi suala hili litakuwa ni historia.

Nam. 16

Ukosefu wa Miundombinu ya Kilimo na Gharama kwa Wakulima wa Kibokwa

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 12

Upungufu wa Madaktari Bingwa Mifugo

Mhe. Salma Mohammed Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi wa Wilaya ya Chake Chake – Pemba wameelekeza maisha yao katika Sekta ya Ufugaji. Kwa kuwa Wizara ya Mifugo Pemba haina madaktari bingwa wa mifugo na zaidi hutegemea madaktari wake katika ngazi ya stashahada (Diploma) ambao karibuni wengi wao wanastaafu. Je, wizara inalitambua tatizo hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 12 kwa heshima kubwa kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba, hivi sasa hakuna Daktari wa Mifugo mwenye Shahada (*Degree*) aliyeajiriwa kwa kudumu huko Pemba, ingawa wapo vijana ambao wanasifa ya kutibu mifugo wenye utaalamu na uzoefu huo katika ngazi ya Cheti na Diploma, ambao wanatoa huduma kwa ufanisi.

Hata hivyo, kwa sasa yupo Daktari wa ngazi ya shahada ambaye ameajiriwa kwa Mkataba anayefanya kazi zake Pemba kwa kupunguza ukosefu huu.

Mhe. Spika, masomo ya shahada ya udaktari wa mifugo huchukuwa si chini ya miaka mitano kwa kukamilika kwake na ni sharti kwa mwanafunzi kufaulu vizuri masomo ya sayansi ya kidato cha sita, ili akubaliwe kujiunga na masomo hayo.

Aidha wizara inawakaribisha vijana wenye sifa hizo, ili iwasaidie katika kutafuta ufadhili na itapendeza zaidi kama vijana hao kutoka Unguja na Pemba, kwa ajili waweze kufanya kazi kwa urahisi.

Hivi sasa wapo wanafunzi waliokwisha kupangiwa kuhudhuria masomo katika ngazi ya shahada ya kwanza juu ya masuala ya utabibu wa mifugo kutoka Ofisi zetu za Pemba.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake ametueleze kwamba kuna mtaalamu ambaye ameajiriwa kwa mkataba na mtaalamu huyu nimesikia na hapa Unguja wapo wataalamu wenye elimu kama yake yeye wasiopungua watano. Kwa hivyo, naomba anieleze ni sababu zipi zilizopelekea kukodi mtaalamu kutoka Bara na kuacha wataalamu waliopo Unguja kumpeleka mmoja Pemba?

(b) Kwa kuwa na wataalamu ni moja ya maendeleo katika nchi na hivi sasa tunategemea kuwa na sherehe kubwa ya kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivi serikali haioni aibu kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi bila ya kuwa na wataalamu wa mifugo. Kukodi mtaalamu kutoka Tanzania Bara, je hii ni faida na matunda ya Mapinduzi yaliyoasisiwa na Mzee wetu aliyekuwa na dhamira nzuri?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, mtaalamu kutoka Bara ameekwa kwa mkataba na *SSP*. Lakini ni kweli wataalamu waliopo watano kutoka Zanzibar ni wale ambao wenye nyadhifa kubwa, moja wapo ni Wakurugenzi pamoja na Katibu Mkuu wetu ambao ndio *specialists* wa mambo yale. Vile vile hivi sasa tunao wataalamu wawili kutoka katika Chuo cha *Agaton* ambao wanarudi hivi karibuni na tumewapangia mmoja kuweza kufanyakazi zake Pemba na mwengine Unguja.

Mhe. Spika, kama hiyo haitoshi pia hivi sasa tunaye mtaalamu mmoja ambaye amesharudi na ameshafika Pemba na wakati wowote tunaweza kumpangia kazi. Lakini si aibu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kusema imetimiza miaka 50 kuwa haina wataalamu.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba wizara hii mpya na muono wa Mhe. Rais ulipelekea kuweka ukaribu zaidi wa wafugaji na wizara yao na sasa wizara imejipanga vizuri na mara hii imetoa zaidi ya wafanyakazi 6 kwenda kusoma *degree* ya mwanzo kwa ajili ya kufaidisha na kutimiza miaka 50 kama alivyosema Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza ninamshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri tena ya kuridhisha kabisa.

Lakini napenda nimuulize kwa sababu wataalamu pamoja na hawa madaktari wa cheti na diploma wadogo wadogo waliopo, ambao ni madaktari wa hii mifugo.

Kwa kweli hawa madaktari waliopo hao wadogo wadogo ofisi zao bado haziridhishi na wakati wa bajeti alituahidi kwamba ofisi hizi zitafanyiwa matengenezo kwa kuwekwa *furnitures* pamoja na vitu vyengine.

Sasa je, suala hili limefikia hatua gani, yaani tayari limeshafikia kiwango na kama bado ni lini hasa hizo ofisi zao zitatengenezwa ili ziridhishe na wale waliopo pale wadogo wadogo wajisikie kama wanafanyakazi katika serikali wakiwa kwenye hali nzuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, bajeti tayari imepita juzi tu na kupanga ni kuchagua. Sasa tumepanga kuelekeza nguvu zetu huko katika hii *quarter* ya mwanzo na bado haijamalizika. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Mwakilishi astahamili kidogo na kazi zetu ataziona na akae mkao wa kula. *(Makofi)*

Nam. 37

Uvamizi wa Ofisi za Serikali na Kupatiwa Hatimiliki

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Wakati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanatembelea ofisi za wizara mbali mbali za serikali hasa zile zilizopo maeneo ya shamba au vijijini, wamekuta sehemu nyingi hazina hatimiliki na hivyo baadhi ya wananchi huvamia sehemu hizo.

Je, serikali kupitia wizara hii itachukua hatua gani za haraka kutoa hatimiliki ya sehemu hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba yapo baadhi ya maeneo ya taasisi za Serikali ambayo yamekuwa yakivamiwa na watu na ni kweli pia yapo baadhi ya maeneo ya serikali ambayo hayana hatimiliki.

Kupitia utekelezaji wa Tamko la Serikali la Majengo ya Taasisi za Serikali na Maeneo yote ya Serikali yasajiliwe na kupatiwa hatimiliki, wizara yangu inaendesha zoezi katika mikoa yote mitano ya Zanzibar la kumtambua mwenye haki ya matumizi ya ardhi na hatimaye kupatiwa hatimiliki.

Aidha, wizara yangu imekuwa ikipima na kutoa hatimiliki na za ukodishaji ardhi kwa Taasisi za Serikali Mijini na Vijijini, ambapo baadhi ya taasisi zifuatazo zimeshafaidika na zoezi hilo.

i) Wizara ya Afya kwa eneo la Kivunge Wilaya ya Kaskazini A, Binguni Wilaya Kati na Makunduchi Wilaya ya Kusini Unguja.
ii) Wizara ya Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto
iii) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano
iv) Idara ya Usalama wa Taifa – Zanzibar
v) Mamlaka ya Ukusanyaji Mapato Zanzibar; na
vi) Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini “B”

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu ya swali lake mama haoni kwamba kucheleweshwa kutolewa hatimiliki katika sehemu zile za serikali ni kuwapa nafasi wale wavamizi wanaovamia ardhi na kuivamia zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kuwapa wananchi hati za umiliki wa ardhi ni kuiondoa migogoro ya ardhi ambayo imetukabili kwa kipindi hichi hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, wizara yangu baada ya kuliona hili imeamua rasmi kwamba kuzifanyia usajili ardhi zote zilizokuwepo Zanzibar kwa ajili ya kuondoa migogoro ya ardhi Zanzibar na kuiondoa migogoro hiyo, basi ni kuzitambua ardhi hizo na kila yule anayestahiki kuitumia ardhi ile basi apatiwe hatimiliki kwa ajili ya kuondoa migogoro hiyo na kumhalalashia matumizi hayo ya ardhi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo tu ambalo ataweza kunisaidia.

Katika jibu la swali mama Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba wizara yake iko katika utaratibu wa kuweza kutoa hati ambapo maeneo kama yalivyoelezwa na

Mhe. Abdi Mosi Kombo. Je, Mhe. Waziri kuna maeneo ambayo hivi sasa yanamilikiwa na maskuli na kwa utaratibu ulivyo ni kwamba huwezi ukapewa hati mpaka eneo lile lipimwe na ulipe fedha kwa ajili ya upimaji. Hali hii ya kuwatoza watu wa skuli wakati ni chombo kile cha serikali ni kuwaonea au kufanya njia hiyo lile eneo wananchi waje kuliteka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba wizara yangu itafuatilia na tayari imeshaanza kufuatilia katika usajili huo wa ardhi ikiwemo maeneo ya skuli, ya raia pamoja na maeneo mengine ya serikali kwa kupitia MKUZA II. Vile vile hivi sasa tayari tumeshaanza katika Wilaya ya Kaskazini 'A' pamoja na Wilaya za Kaskazini Pemba.

Kwa hivyo, tunachotegemea ni kufanya upimaji na tayari upimaji umeshafanywa kwa baadhi ya maeneo ndani ya wilaya hiyo na tunategemea kutoa hati bila ya kumtoza mtu kodi kwa kupitia mradi huu, isipokuwa tutapima na baadaye tutamkabidhi hatimiliki kama ni haki yake ya matumizi ya ardhi hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja kama ifuatavyo. Kutokana na serikali kuchelewa kutoa hatimiliki hasa kwa skuli wananchi wamechukua nafasi hiyo ya kujenga maeneo ya skuli sana. Je, serikali ina mpango gani baada ya kutoa hatimiliki kwa wananchi wale ambao tayari wameshachukua maeneo ya skuli?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali imechelewa katika ufuatiliaji huo wa kuzisajili ardhi katika maeneo hayo ya mashamba. Kwa kweli niseme kwamba imechelewa kwa sababu maalumu, kwa sababu suala hili linahitaji fedha za kutosha kwani ni suala linalohitaji gharama, ili utekelezaji huo basi lazima tuwe na fedha ambazo zitakazotumika kwa ajili ya shughuli hizo na tunategemea wafadhili kutusaidia kama tunavyoendelea na mradi huu *phase* ya pili ya MKUZA.

Kwa hivyo, niseme ni kweli imechelewa, lakini uchelewaji wa serikali si kwamba wananchi hao hawatapata haki ya kufanyiwa mipango miji katika maeneo yao. Kwa maana hiyo, tunategemea kwamba tutawapangia wananchi na tutafanya marekebisho kwa wale wote ambao wamejenga nyumba zao kinyume na utaratibu stahiki.

Nam. 96

Maeneo ya Biashara Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Vijana wengi wameamua kujitafutia kipato kupitia sekta ya biashara lakini hadi sasa wamekuwa wakifanya biashara katika mazingira magumu kutokana na kukamatwa kila mara bidhaa zao na kushitakiwa na Manispaa ya Zanzibar.

(a) Serikali ina mpango gani wa kutenga maeneo maalumu ikiwemo kujenga maduka maalumu ya wafanya biashara wadogo Zanzibar?

(b) Wizara ya Biashara ina mpango gani na eneo la Bwawani na Makontena ya ukanda wa Darajani kujengwa majengo ya maduka ya kisasa ili kuondoa tatizo la bidhaa kupangwa chini ya kituo cha daladala Zanzibar?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 96 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga eneo maalumu la Saateni kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo na ina mpango wa kuliendeleza eneo hilo ili kuweza kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara hao.

Katika kuliendeleza eneo hilo serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na kutafuta utaratibu wa kudumu wa kuweka miundombinu ya uhakika ya umeme na maji, vyoo, pamoja na kutenga maeneo ya kujenga Kituo Kidogo cha Polisi na huduma nyengine muhimu, ili liweze kuvutia kwa wafanyabiashara kufanya biashara zao katika eneo hilo zaidi kibiashara. Ni azma ya serikali Mhe. Spika, kuliendeleza eneo la Saateni ili kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo.

(b) Mhe. Spika, kwa kuliendeleza eneo la Bwawani kwamba kunahitaji kiwango kikubwa cha fedha na serikali inatafuta wawekezaji, kwa ajili ya kuliendeleza eneo hilo la Bwawani. Madhumuni makubwa ni kulifanya eneo hilo kuwa la biashara hapa Zanzibar.

Katika mpango huo Serikali ya Mapinzudi ya Zanzibar inakusudia eneo hilo pamoja na kufanya shughuli za biashara pia kuwe na kumbi za mikutano (*conference halls*), shughuli za uendelezaji wa masuala ya mahoteli pamoja na kujenga mikahawa (*cafeteria*) na sehemu ya kuchezea watoto (*children parks*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kusikitisha, Baraza hili hili si mara ya kwanza, si ya pili wala si ya tatu tumekuwa tukiambiwa kwamba eneo la Saateni ni eneo la kujengwa Bandari ya Mpigaduri, sasa leo jambo la kusikitisha ni kwamba serikali inataka kutia nguvu zake zote pale.

(a) Kuhusiana na suala hili Mhe. Naibu Waziri anatoa kauli gani, inaonekana kwamba wafanyabiashara hawa hawajui pa kukamata. Kwa kweli eneo lile lile tumeambiwa humu katika Baraza hili kwamba eneo lile itajengwa Bandari ya Mpigaduri. Lakini leo panataka kujengwa Kituo cha Polisi, huduma za maji pamoja na vyoo au ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri haupo?

(b) Serikali inatekeleza vipi Sera ya Mfanyabiashara Mdogo, ili awe mkubwa, kwa sababu tunashuhudia mara kwa mara wafanyabiashara wadogo wadogo kufukuzana na askari na wengine kupoteza vitu vyao na hata wengine kunyang'anywa?

Kwa kweli hichi ni kitendo cha kusikitisha tena cha kutia aibu, ukizingatia ajira yenyewe haipo na wengine wamekopa fedha benki kwa ajili ya kujiendeleza na leo wanafukuza mule vichochoroni na askari. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Naibu Waziri angetueleza ili wananchi wapate kufahamu ukweli wa suala hili uko vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, mpango wa kulifanya eneo la Saateni kuwa ni Eneo la Bandari Huru suala hilo lipo na linazungumzwa, lakini kwa sasa kwa sababu tayari wapo pale wafanyabiashara wadogo wadogo kuwapelekea huduma hizi muhimu Mhe. Spika ndilo tunalolizungumzia, kwa sababu kuna mipango ya *long-term, medium and short-term*. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe aelewe hivyo. *(Makofi)*

Kuhusu suala la wafanyabiashara wadogo wadogo kubughudhiwa na askari kwenye biashara zao. Mhe. Spika, hakuna nchi inayoendeshwa bila ya utaratibu wanapokaidi maelekezo ya serikali inabidi nguvu za ziada zichukuliwe. Lakini

naamini kabisa kwamba kama watafuata maelekezo wanayopewa wafanyabiashara wadogo wadogo, basi suala la kubughudhiwa na askari litakuwa halipo.

Kwa hivyo, sisi tukiwa kama viongozi ni wajibu wetu kuwaelekeza wafanyabiashara hawa kwamba nchi yoyote inaendeshwa kwa utaratibu na ni vyema kufuata taratibu tunazoekewa, ili kuepukana na kero ndogo ndogo za aina hiyo Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu viwili kama ifuatavyo.

(a) Iwapo wafanyabiashara wadogo wadogo wanakiuka taratibu kama alivyosema ni sheria ipi ya nchi hii inayoruhusu kutaifishiwa mali zao?

(b) Kwa sababu nyimbo ya kupeleka huduma za jamii ambazo ni za msingi katika eneo la Saateni imekuwa ikitolewa na serikali kwa takribani zaidi ya miaka 10 tangu wafanyabiashara hawa walipohamishiwa katika eneo lile. Kwa hivyo, ni lini serikali itaacha ahadi isiyotekelezeka na kuyatekeleza yale ambayo wanayoyaahidi katika Baraza hili na nje ya Baraza? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Spika, kwa idhini yako kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa majibu yake namna alivyoyatoa.

Pili, Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka nimthibitishie kwamba hakuna sheria yoyote ile inayoruhusu mtu kunyang’anywa haki yake bila ya utaratibu maalumu.

Pili, pia nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba wafanyabiashara wadogo wadogo waliopo Juakali mimi mwenyewe binafsi pamoja na taasisi ninazoziongoza katika kipindi kama cha mwezi mmoja nyuma, tumekuwa tukiwaelimisha namna gani wanaweza wakaondoka na kwenda kulitumia eneo la Saateni kwa ajili ya kufanya biashara ndogo ndogo.

Mhe. Spika, eneo la Saateni hivi sasa kuna wafanyabiashara wasiozidi 200 na eneo la lenyewe lina uwezo wa kubeba wafabiashara wadogo wadogo wapatao 600. Kutokana na hali hiyo, niendelee kuwaomba wafanyabiashara wadogo wadogo waliopo Juakali kwamba waende Saateni kwa ajili ya kufanya biashara zao. Katika

eneo la Darajani hairuhusiwi kufanyabiashara kwa wale ambao hawana maduka ya kufanyia biashara zao.

Kwa hivyo, ili kuepukana na hasara hizo ndio maana serikali imekuwa ikitoa taaluma juu ya wafanyabiashara kuwasihi kwamba waende Saateni kwa ajili ya kufanyabiashara zao.

Mhe. Spika, hakuna nyimbo ambayo inaimbwa siku zote na serikali juu ya kupeleka huduma muhimu. Mhe. Spika, mimi baada ya uteuzi wangu nililitembelea eneo la Saateni na nilibaini kasoro zilizopo na baada ya kuzibaini kasoro hizo huduma ambazo zinahitajika kupelekwa kwanza ni huduma ya maji, vyoo, umeme pamoja na ulinzi kwa ajili ya bidhaa zitakazokuwepo Saateni ambazo zitahifadhiwa katika ghala maalumu ambalo limejengwa kwa muda mrefu sana na Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba huduma ya maji tayari ipo, umeme ulikuwepo wenye voltage ndogo tayari tumeshawasiliana na Shirika la Umeme kuweka umeme mkubwa, ili kuwa na mwanga mkubwa zaidi kwa ajili ya kuepusha vibaka wadogo wadogo kwenda kudokoa biashara za wafanyabiashara. Vile vile huduma za vyoo tayari tumeiimarisha na vipo vyoo vya kutosha.

Pia, kuhusu jengo la askari, lilikuwepo jengo ambalo lilitengenezwa kwa ajili ya ofisi kama ni *Market Master*, hivyo jengo lile sasa tumeamua liwe ni Kituo Kidogo cha Polisi. Kwa hivyo, askari kwa maana ya Kamati ya Ulinzi na Usalama inayowashirikisha askari polisi, JKU, Valantia, KMKM, Magereza na Faya wapo pale kwa ajili ya kuimarisha ulinzi ili bidhaa za wafanyabiashara zisiweze kupata matatizo, lakini vile vile na kulinda usalama wa eneo lile.

Nataka nitumie fursa hii Mhe. Spika, kuwaomba wafanyabiashara wote wa Juwakali waelekee Saateni, na kuanzia tarehe 1/11/2013, hakuna Mswalie Mtume, askari wetu watafika pale, ili kuepukana na hilo suala la kusema kwamba wanaibiwa mali zao ni vizuri wasipeleke bidhaa pale, askari wetu watafika mapema na hakuna mtu atakaefika pale kuweka bidhaa. Nawaomba tena na nawasihi, hakuna *compromise*, hakuna mazungumzo wala hakuna mtu yeyote ambaye anaweza akasitisha haya maamuzi ya serikali.

Jengine serikali inampango gani? Pale Saateni ni pahala ambapo patafanyiwa biashara kwa muda kwa kuelewe hiyo mipango mikubwa ya serikali ya kujenga bandari. Kwa hivyo pale tupo kwa muda na serikali imeamua kutafuta eneo

maalumu kwa ajili ya kujenga Juakali Complex ya kudumu katika maeneo ya Mwanakwerekwe ambalo jengo litakuwa la kudumu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Ahsante sana Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba tusaidie tukamate jibu lipi kwa sababu utaratibu serikali inajibu inategemea majibu yake itakuwa yamezingatiwa kwa pamoja chini ya msingi wa uwajibikaji wa pamoja. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba serikali ina mpango wa kupeleka huduma ambazo alizitaja. Mhe. Waziri aliyekaa anatwambia serikali imeshapeleka huduma zote zipo. Tuchukue jibu lipi katika haya mawili Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Nafikiri Waziri anayehusika na pale hasa ni Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum, nategemea yeye atakuwa anaelewa zaidi juu ya jambo hilo. Nadhani tuendelee isiwe mabishano.

Nam. 8
Uendeshaji wa Hoteli ya Bwawani

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-
Hoteli ya Bwawani ni hoteli pekee kubwa iliyojengwa na Serikali yetu ya SMZ katika miaka ya 1970 kwa ajili ya Biashara na ilipokea wageni wa nje na ndani ya nchi kwa uadilifu mkubwa. Kwa kuwa kuna taarifa kwamba Hoteli hiyo imepoteza mwelekeo asilia wa kutoa huduma za malazi na chakula kwa wageni na kujiingiza katika shughuli nyengine jambo linalorudisha nyuma maendeleo ya Hoteli hiyo.

a) Je, ni kweli kwamba Afisi ya Mkuu wa Wilaya wamehamishia Afisi zao ndani ya majengo ha Hoteli hiyo?
b) Kama ni kweli ni malipo kiasi gani taasisi hiyo wanalipa kwa mwezi?

c) Kwa kuwa Biashara ya Kitalii na Uendeshaji wa shughuli za kiofisi ni vitu vinavyohitaji utafiti mkubwa, Je, kuwepo kwa Afisi hizo hotelini hapo si kuirudisha nyuma Hoteli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo - Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza sio kweli kwamba hoteli hiyo imepoteza muelekeo wa kutoa huduma za malazi na chakula, bado huduma hizo zinaendelea...

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mimi ndiye ninaejibiwa swali langu lakini kwa mujibu wa sauti ilivyo sisikii jibu naomba aongeze sauti.

Mhe. Spika: Haya jitahidi na kuielekea hiyo maiki ili tusikie sote. Mhe. Naibu Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza sio kweli kwamba hoteli hii imepoteza muelekeo wa kutoa huduma za malazi na chakula, bado huduma hizo zinaendelea.

a) Mhe. Spika, ni kweli Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini hivi sasa iko kwa muda katika hoteli ya Bwawani baada ya kukodi na kutumia vyumba vitano. Tokea kuhamia katika hoteli hiyo Ofisi hiyo inatakiwa iwe imelipa shilingi milioni ishirini sawa na shilingi milioni moja kwa mwaka. Hata hivyo hadi hivi sasa ofisi hiyo bado haijalipa na tunategemea italipa ndani ya kipindi cha mwaka huu wa fedha. Hivyo fedha hizo zimewekwa kuwa kama deni la ofisi hiyo.

b) Mhe. Spika, ni kweli biashara ya kitalii na uendeshaji wa shughuli za kiofisi ni vitu vinavyohitaji utafiti mkubwa. Utafiti wa biashara ya kitalii na hasa kwa hoteli unalenga zaidi upatikanaji wa wateja wa kutosha wa kujaza vyumba muda wote wa mwaka.

c) Mhe. Spika, inapotokea fursa ya vyumba vya hoteli kukodiwa kwa mwaka mzima iwe kwa kulala wageni au kwa kufanya ofisi hiyo ni kuelekeza shughuli za hoteli na sio kurudisha nyuma mradi tu. Ulipaji unafanyika kama inavyotakiwa ni matengemeo kwamba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini na nyengine zitakazopanga kwenye hoteli hiyo zitalipa kama kawaida na kutekeleza wajibu wao unaohusika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri katika masuala haya ya habari, utamaduni na michezo, huyu Saidat Naibu Waziri (bi Hindi) naomba kuuliza swali dogo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ipo pale na ina vyumba vitano na mpaka hivi leo kodi haijalipwa. Na kwa kuwa wakati sisi tunajenga Hoteli ile Mheshimiwa lengo letu sisi ilikuwa ni kutoa ajira kwa vijana wetu pamoja na kuwaongezea kipato. Hoteli ile iliajiri zaidi ya vijana 200 kipindi kile cha miaka ya 70 moja kwa moja au kwa kupinda tu kidogo, aidha kuwaajiri vijana au kuchukua mazao ya wakulima ikawa tununue pale, jambo ambalo lilipunguza umasikini kwa kiwango kikubwa kwa wananchi wetu.

Je, kutoa vyumba vitano ukawapa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya huku wakipiga type, huku wakifanya zogo, watalii pale wataendelea kubaki pale, huko si kuwatorosha wateja wetu katika ile hoteli kwa kufanya hivyo si kupoteza muelekeo wa kihoteli?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi nimetoa ufafanuzi wa kutosha kwa sababu nimejibu hoteli yetu kwamba haipotezi muelekeo na inatoa huduma za kula na malazi na haitoi usumbufu wowote kwa wageni kuwepo ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo sana pamoja na majibu yake mazuri sana. Mheshimiwa ameeleza moja ya Ofisi ya Wilaya tu ambayo ina vyumba vitano.

a) Atakubaliana na mimi kuwa kuna ofisi nyingi kuliko hizo Ofisi alizozitaja tano ambazo ni watu mbali mbali, wanashughuli ambazo hazilingani na utalii?

b) Mhe. Spika, Mhe. Waziri umesema kuwa Wilaya hailipi kodi mpaka leo hii inadaiwa. Je, huoni ipo haja sasa hawa watu kwa kuwa wamevunja mikataba hawalipi suluhisho ni kuwaondoa mara moja?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kuwa na nyie Waheshimiwa Wawakilishi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuna Ofisi zenu Hoteli ya Bwawani. Waheshimiwa Wawakilishi kama alivyoniuliza Mhe. Mshimba Mbarouk, Mkuu wa Wilaya analipa lakini kipindi hichi cha mwaka huu ndio sasa hivi ataanza kuendelea na kulipa wakati wa bajeti hii iliyopita. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi muwe tayari na nyinyi mnaokodi pale mlipe, msilalamikie Ofisi ya Mkuu wa Wilaya tu. Yeye Mkuu wa Wilaya tayari tumefungina mkataba na atalipa na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mpo pale mlipe.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, Mheshimiwa Naibu katika swali langu alilonijibu alisema kuwa na Waheshimiwa wamo katika maeneo yale ambao wameekeza katika Ofisi. Naomba Mheshimiwa atutajie Waheshimiwa gani waliyokuwepo pale katika sehemu ile.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hilo si kuhusu utaratibu, hilo ni suala jengine la nyongeza.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa vile ulikiri kwamba kuna baadhi ya taasisi ambazo kuwa hazilipi, ukiachilia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini ni taasisi ngapi nyengine ambazo zimekodi katika Hoteli ya Bwawani na malipo yake yakoje?

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kabla ya kumjibu Mhe. Farida kwanza naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wangu kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, suala la hoteli ya Bwawani ni Taasisi ya Biashara, kwa hiyo jukumu lake ni kuona namna gani shughuli zake za kibiashara zitakuwa iwe ni kulaza wageni, iwe ni huduma za chakula au huduma nyengine. Hili ni jambo la kawaida sana kwa hoteli. Mara moja pale Dar-es-Salaam hata Ofisi za Kibalozi zilikuwemo katika Hoteli kubwa za pale Dar-es-Salaam. Nakumbuka hata Hoteli ya Kilimanjaro kulikuwa kuna Ofisi za Kibalozi zilikuwa zimepanga pale. Kwa hivyo hili ni jambo la kawaida Waheshimiwa Wawakilishi kwa hoteli za kitalii.

Kwa hivyo hivi sasa ni kweli Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ipo pale ina vyumba vitano, tuliwahi kuzungumza na Mheshimiwa aliyekuwa Waziri hapa kwamba atulipe na amepanga kulipa katika Bajeti hii na ahadi hii imerithiwa na Mhe. Waziri anayeshughulikia Tawala za Mikoa hivi sasa kwamba ameahidi katika bajeti hii tunayokwenda nayo basi deni ambalo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inadaiwa itatulipa.

Nikija suala hili la Mhe. Farifa mbali ya vyumba vitano ambavyo Mhe. Mkuu wa Wilaya amekodi kuna vyumba vyengine 17 vimekodiwa na taasisi mbali mbali za kibiashara katika eneo lile lwa Bwawani. Kwa hivyo, jibu lake ni kwamba ni taasisi mbali mbali za kibinafsi na za kiserikali ikiwemo hata Kamisheni ya Utalii

pale ipo, ZFA na maeneo mengine. Lakini ninachokieleza kwa Baraza hili tukufu kwamba taasisi nyengine zinalipa kodi zao kwa kawaida kila mwezi na nyengine zimelipa *in advance* yaani wanatudai sisi.

Kwa hivyo, ni Ofisi ya Mkuu wa Wilaya tu ndiyo ambayo kidogo ilikuwa na matatizo lakini mawaziri wote wawili yule aliyetoka na yule ambaye ameingia wote wameiahidi wizara yangu kwamba katika mwaka huu wa fedha deni lao watalimaliza.

Nam. 46

Ahadi ya Ajira kwa Vijana wa *Redcross*

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa vijana wetu wa *'RED CROSS'* katika kujitolea kufanya kazi ya usafi katika wodi na kazi nyenginezo katika hospitali za Serikali (Unguja na Pemba) Mhe. Waziri aliahidi kuwa vijana hao watakuwa ni wa mwanzo kupatiwa ajira ambazo wanazimudu wakati ajira hizo zikitolewa.

a) Je, ahadi hii ilikuwa ya kweli na Mhe. Waziri ana maelezo gani kuhusu vijana hawa?

b) Ni sababu zipi zilifanyika vijana hao kutoajiriwa katika ajira zilizotolewa mwezi wa Julai, 2013 na badala yake wakaajiriwa vijana wengine kabisa?

c) Mhe. Waziri haoni kuwa kwa vijana hawa kutopatiwa ajira hizi ni kutowatendea haki kwa vile walishaingiwa na tamaa ya kupatiwa ajira hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, *Red Cross* ni kikundi kinachoshughulika na huduma ya kwanza katika mikusanyiko mbalimbali ya watu. Ili waweze kumudu kazi zao vyema, wakeshajifunza nadharia huomba kufanya mazowezi kwa vitendo katika mahospitali na vituo vya afya kwa muda maalumu. Kilichowafanya wabakie vituoni baada ya muda wao waliopangiwa kwisha ni upungufu wa wahudumu katika sehemu hizo na ndio chimbuko la kujitolea kwao.

Kabla ya Sheria ya Uajiri Serikalini kifungu cha 57 (3)(a)(b) na (c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 ambayo tumepitisha sisi hapa tuliopo Barazani kila wizara ilikuwa inaajiri wafanyakazi wake wenyewe na ndio maana ahadi hiyo ikaweza kutolewa. Baada ya Sheria hiyo kupitishwa, jukumu la uajiri lilikabidhiwa Tume ya Utumishi Serikalini na ikaweka taratibu maalumu za watu kuajiriwa, ikiwa ni pamoja na kutangaza nafasi za kazi kutangazwa katika vyombo vya habari vya umma ili wenye sifa waombe.

Kwa Sheria hiyo uwezekano wa wizara kuajiri ukashindikana hata kama waliahidiwa. *Red Cross* waliarifiwa hilo na kupewa maelekezo waombe kazi kupitia Tume itapotangaza nafasi hizo. Matangazo ya ajira yalipotoka watu waliomba pamoja na hao wa *Red Cross,* lakini si wote waliweza kupita kwenye usaili. Mhe. Spika, vijana hawa ingekuwa hawakutendwa haki kama wangekuwa hawakuelezwa utaratibu na sheria zilivyo na wasingeambiwa kuomba kazi Tume.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa maelezo yake ya ukweli ambayo kauli hasa ya Mhe. Naibu Waziri ilibadilika baada ya sheria Nam 57 Kifungu cha 3 (a), (b) na (c) kama alivyoeleza Mhe. Waziri.

Pamoja na kuwa Mheshemiwa amesema ajira ilipokuwa tayari tangazo lilitokea na watu wakaomba na kujaza fomu na miongoni mwao wale vijana wa Red Cross wengine walipata na wengine walikosa.

a) Walikuwa ni vijana wangapi wa *Red Cross* na ni wangapi wa walipata katika usaili na kuajiriwa na ni wangapi walikosa.

b) Hao waliokosa ni kwa sababu nafasi ilikuwa hazimo tena kwa wale waliotaka kuajiriwa au ni kwa sababu hawakupasi inter view hizo.

c) Kama ni sababu ya nafasi hawa wamo katika mazingira gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, watu waliokuwepo kwenye Red Cross walianza kuajiriwa kwa awamu tatu tofauti kuanzia mwezi wa Mei mpaka mwazi wa Julai nafasi tofauti.

a) Waliokuwa wakijitolea na kuajiriwa kwa wote walikuwa ni 55 wa *Red Cross,* kati ya hao waliopata Unguja ni 40 na waliopata Pemba ni 15 na jumla waliobaki ambao waliokuwa wakijitolea kama *Red Cross* na wasiokuwa *Red Cross* kwa sababu katika kujitolea kulikuwa na makundi mawili kuna wale wa *Red Cross* na wengineo waliokuwa wamejitolea walikuwa ni 103, kutoka Unguja ni 53 na kutoka Pemba ni 50.

b) Sasa hawakuajiriwa kwa kuwa hakukuwa na nafasi, hapana nafasi zilizotolewa ajira zilikuwa nyingi kwa ajili ya Unguja na Pemba zilikuwa ni nafasi 245, lakini usaili ulishindwa kuwapitisha hao. Kwa sababu katika nafasi 245 watu waliokuwa wameomba ajira walikuwa ni elfu na zaidi. Kwa hivyo usaili ulipopitishwa tukapewa watu 245 tuliowaomba wakiwemo watu wa kawaida, wakiwemo waliojitolea, wakiwemo *Red Cross*. Lakini nataka nikwambieni kabisa kwamba wote ni Wazanzibari hakuna mtu wa nje na wote walikuwa na haki ya kuajiriwa kwa mujibu wa sheria kwa hivyo ni usaili ndio uliowatowa hawa. Kwa hivyo, sina nafasi wala mazingira iliyowafanya watoke isipokuwa usaili ndio ambao uliotenda haki na sina tena nafasi kwa ajili ya *orderly* kwa hivyo nisiambiwe niwachukue maana pa kuwaweka sina.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye ufasaha mkubwa sana. Swali langu lipo hapa.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Waziri baada ya kufanya marekebisho ya sheria hasa katika mambo ya utumishi, vigezo sasa hivi moja kwa moja vinakwenda katika sifa kwa zile taasisi ambazo sehemu ambazo zilizotangazwa. Kwa kuwa kumekuwa na utaratibu katika taasisi zetu mbali mbali za serikali na utaratibu huo ulikuwa kama serikali ina uhaba wa wafanyakazi ilikuwa inawachukua baadhi ya vijana kwa ajili ya kujitolea, lakini kwa bahati walikuwa wanawapa matumaini kwamba watawapatia ajira pale zitakapokuja. Sasa kwa kuwa baada ya kufanya marekebisho ya sheria nafasi ile sasa hivi kwa serikali imekuwa ndogo kwa sababu kitu kikubwa kinachoangaliwa zaidi ni sifa za wale wanaotakiwa kuajiriwa.

Je, serikali kwa kuwa bado kuna vijana wengi katika taasisi mbali mbali ambao wanaendelea kujitolea na wamekwisha kuahidiwa kwamba wataajiriwa je, serikali ipo tayari kutoa tamko au kuwapa maandishi vijana wale katika taasisi mbali mbali ili sasa kuondokana na ile dhana wa ile ahadi waliyotolea na wajipange aidha katika kujisomesha zaidi ili zitakapokuja zile nafasi za ajira waweze kufaulu kwa mujibu wa ushindani wao?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Wizara yetu ya Afya baada ya tu kubaini tu kwamba uwezekano wa kuwaajiri hatuna, mimi binafsi nimewaita Wakurugenzi, nikawafahamisha hilo, nikatoa dokezo kwa Wakurugenzi nikawaambia kwamba kwanza wawasimamishe watu wote wanaojitolea kwa sababu sina dhamana nao tena. Lakini la pili nikawaambia baada ya

kuwasimamisha wale wanaojitolea nikawambia kwamba wasiruhusu tena mtu kujitolea ambaye hakuajiriwa katika Wizara kwa sababu mbili za msingi.

Kwanza sina dhamana ya kumuajiri kwa sababu kajitolea. Pili mtu tu kuingia katika wizara ambaye hakuajiriwa usalama ni mdogo, anaweza akatufanyia chochote na pa kumkamatia hatuna. Kwa hivyo, sikutaka na tangazo nilitoa na wote *Red Cross* walikuwepo, walilijua hilo na wote walitoka. Nasikia Pemba kuna waliokuwa wamebaki, sasa kama wamebaki ni udhaifu wa viongozi wa Pemba na hao waliokuwepo Pemba ni kwa matakwa yao. Lakini waliambiwa wote waache nilitoa tamko na kuanzia sasa hakuna mtu atakayejitolea katika Wizara ya Afya.

Nam. 109

Kukamatwa kwa Meli ya MV Gold Star Iliyosajiliwa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, nimpe pole Mhe. Naibu Waziri. Septemba 9 mwaka huu Meli ya MV Gold Star ilikamatwa na bangi yenye thamani ya shilingi billioni 125 katika mwambao wa bahari ya Italy ikiwa imesajiliwa Zanzibar kupitia wakala wake maarufu Kampuni ya *Philtex* na kuharibu jina la Tanzania.

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua gani dhidi ya Kampuni iliyohusika na usafirishaji wa dawa hizo za kulevya kinyume na masharti ya leseni ya usajili wa meli?

(b) Kampuni ya *Philltex* inatumia vigezo gani kabla ya kusajili meli kutokana na kuwepo malalamiko ya kusajiliwa meli chakavu na zenye vikwazo katika Baraza la Usalama la umoja wa Mataifa?

(c) Mamlaka ya usafiri Baharini imenufaika kiasi gani cha mapato kwa kila mwaka tangu kufunga mkataba na wakala wa kusajili meli Dubai, Kampuni ya Philltex mwaka 2007?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 109 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba nipokee pole yake kwa niaba ya Wizara. Pia naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo. Kama tunavyofahamu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inasajili meli kwa mfumo wa usajili wa ndani na usajili wa nje. Katika usajili huo taratibu husika pamoja na sheria za nchi lazima zizingatiwe katika zoezi hilo, hivyo likitokea tatizo lolote Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitosita kuchukua hatua stahiki kwa mtendaji huyo.

Mhe. Spika, kama maelezo ya swali yanavyojieleza tayari kutokana na kadhia ilivyojitokeza Zanzibar *Mari Time Authority* imechukua hatua za kinidhamu juu ya jambo hili, hatua ambayo ni kuifutia usajili kwa meli ya MV Gold Star kwa kutambua kwamba kitendo walichokifanya cha kupakia bangi ni kinyume na taratibu za kisheria za usajili wa meli na miongozo ya IMO duniani.

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar imechukuwa hatua ya kuifutia usajili Meli ya MV Gold Star mara moja kama tulivyoeleza hapo awali.

(b) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar inayo mikataba na Makampuni au Taasisi yaani zile za *(classification Societies)* zinazofanya ukaguzi wa meli za nje kwa makubalino ya kufanya kazi kwa kushirikiana na Kampuni ya *Philtex*. Meli zinazosajiliwa huwa zimetimiza masharti na vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Usajili. Aidha Mamlaka haisajili meli chakavu na meli iliyochini ya viwango vya ubora au vikwazo kwa mujibu wa maelekezo au Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, pale inapotokezea wakala akiwa amefanya makosa kama hayo kusajili meli bila ya kufata taratibu au bila ya kupata taarifa za kina kuhusiana na meli hiyo iliyosajiliwa, mamlaka huchukua hatua za kuufuta usajili huo mara moja.

(c) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar kupitia Wizara iliyokuwa ya Mawasiliano na Uchukuzi ilisaini mkataba na Kampuni ya Philtex tarehe 04/03/2007 kabla ya kuanzishwa kwa Mamlaka husika. Mkataba huo bado ni wa Serikali na Kampuni hiyo. Mapato yote yaliyokuwa yakipatikana yalikuwa yakilipwa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kutambua kwamba hakukuwa na chombo maalumu kilichokuwa kikiingiza na fedha hizo zilikuwa zikiingia Hazina.

Hata hivyo napenda kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba baada ya kuundwa kwa Mamlaka na kuanza kazi rasmi tarehe 1/7/2012 kwa mwaka wa fedha uliopita yaani mwaka wa fedha 2012/2013 Mamlaka imenufaika kwa kuweza kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni 411,774,550 kutoka kwa wakala wa usajili wa meli Dubai kwa Kampuni ya Ciltech.

Mhe. Spika: Ninasikitika muda wa maswali umemalizika. Waheshimiwa Wajumbe tuna kazi ya kupitisha miswada miwili ambayo bado ninaelewa kwamba tuko kwenye kusherehekea sikukuu ya Alhajj, sasa nimepanga na Mawaziri wanaohusiana na miswada hiyo wajiweke tayari vizuri ili kazi hiyo imalizike kipindi hiki cha asubuhi, jioni tukapumzike. Na kwa maana hiyo wale walioko nje sasa waingie ndani tuje tukamilishe hii kazi iliyobaki, ili baadae tuendelee na sherehe za sikukuu ya Idd.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuandikwa Upya Sheria Inayohusu Kampuni na Jumuiya Nyengine, Kuweka Masharti Madhubuti Zaidi ya Utaratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuiya na Mambo Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumemaliza majadiliano kabla ya sikukuu kwa hivyo leo moja kwa moja namuomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Ningewaomba tu waheshimiwa wajumbe wanaokwenda kwa dharura nje wakumbuke kurudi ili kumaliza kazi hii, naomba sana waheshimiwa wajumbe. Tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika kwanza sina budi kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii lakini la muhimu zaidi naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa wazima na kwa kusherehekea sikukuu yetu ya Idd el Hajj, Wizara yangu pamoja na wafanyakazi wake wote tunawaombea wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waendelee na sikukuu njema kwao pamoja na familia zao.

Mhe. Spika, katika mswada huu unaohusiana na makampuni tulipata wachangiaji kumi ambao walichangia kwa kuzungumza na mchangiaji mmoja alichangia kwa maandishi. Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kuwataja wachangiaji wote.

Mhe. Ussi Jecha Simai - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.
Mhe. Abdalla Mohammed
Mhe. Amina Iddi Mabrouk

Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Subeit Khamis Faki
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Mgeni Hassan Juma

Na alochangia kwa maandishi ni Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Spika, kwanza niwashukuru wajumbe wote kwa sababu walikubaliana na mswada wangu na walikubaliana kwamba mswada huu ni mzuri na utasaidia jamii. Lakini zaidi ni mambo mawili muhimu ambayo yalizungumzwa na naomba haya niyazungumze kwa ujumla na baadae nitakwenda katika maelezo mbali mbali ambayo waheshimiwa waliyatoa.

Kwanza Mhe. Spika, naomba nifafanue zaidi kwamba sisi Wizara yetu inasajili makampuni hiyo ndio kazi kubwa. Sasa unaposajili kampuni haina maana kwamba Wizara yetu imeshakupa leseni ya kuanzisha biashara yako, kusajili kampuni ni suala moja na kuanzisha biashara ulizosajili chini ya kampuni hiyo ni suala jengine. Kwa hivyo wale wote ambao wanasajili makampuni wanatakiwa baadae waende wakasajili au wakachukuwe leseni katika Idara au katika sehemu ambazo zinahusika.

Kwa mfano unaposajili Kampuni pengine ya Kuzalisha Madawa, haina maana kwamba sisi tumeshakupa leseni ya kuanzisha hicho Kiwanda cha Madawa lakini baada ya kupata usajili wa kampuni unatakiwa uende katika sehemu inayohusika pengine Wizara ya Afya uombe leseni ya kuanzisha hicho Kiwanda cha Madawa, ili na wao waeleze masharti yao, dawa zao ziwe namna gani, utaratibu wa dawa zile katika ku-*pack* na kufanya kama hayo. Kwa hivyo ni la mwanzo ambalo naomba nilieleze.

Lakini la pili Mhe. Spika, kulikuwa na suala muhimu ambalo lilizungumzwa kwa mfano, majina ya kampuni na hapa tulisema kwamba majina yenyewe Mrajis anaweza akabadilisha. Ni kweli kwamba jina la kampuni linaweza likabadilishwa na Mrajis kwa sababu nyingi tu. Kwa sababu unapoanzisha kampuni na ukaleta katika Ofisi zetu Mrajis anatakiwa atizame lile jina ambalo limeletwa katika kuanzisha Kampuni hiyo.

Na kuna mambo mengi ambayo yanatizamwa pengine jina linaweza likaletwa lakini likawa halikubaliani na utaratibu au na mila za nyumbani. Kwa mfano unapokuja na Kampuni ukasema unataka kuanzisha kampuni ukaiita Kampuni ya Usagaji hili itakuwa haiwezekani na Mrajis ana wajibu wa kubadilisha jina hili. Kwa hivyo ndio hapo tunaposema kwamba Mrajis anaweza akabadilisha jina kutokana na utaratibu ule ili kuleta mantiki halisi ya kampuni ile pamoja na utaratibu mzima wa silka na mila za Wazanzibari.

Lakini la pili Mhe. Spika, watu wengine wanaanzisha kampuni ambazo wanabadilisha kidogo mambo yale ambayo yanafanywa na kampuni nyengine. Kwa mfano kuna Kampuni ya *Panasonic*, sote tunajua kwamba Kampuni ya *Panasonic* ni kampuni mashuhuri, nzuri na vitu vyake ni vizuri. Sasa unaweza ukaja ukaanzisha kampuni husemi *Panasonic* lakini natoa neno moja tu au natoa herufi moja tu bada ya **a** unaondoa **a** unaweka **e** na ikawa *Panesonic*. Sasa mtu wa kawaida anaweza akaona ni Kampuni ile ile ya *Panasonic* na akachukua vitu vyake ulivyoleta vile katika kampuni kwa jina lile lile, yeye anajua kwamba ni *Panasonic* lakini kumbe umedanganya.

Kwa hivyo, Mrajis anapoona mambo kama yale basi anawajibika kuzungumza na wale wanaohusika ili jina liweze kurekebishwa. Kwa hivyo, Mrajis ana mambo mengi ya kutizama. Kwa mfano huduma zinazotolewa, au zitakazotolewa, asili ya mtoa hilo jina, gharama za bidhaa, ukubwa pia wa biashara zile zinaweza zikatizamwa na mambo kama haya.

Mhe. Spika, suala la pili ambalo lilizungumzwa kwa ujumla ni suala la kampuni yenye dhima na kampuni iliyokuwa haina dhima yaani *limited* na *unlimited company*. *Company liability* maana yake ni dhima ya wajumbe wa Kampuni kwa wadeni wake iwapo itatokea Kampuni kufungwa, kampuni inaweza kuwa na dhima yenye ukomo yaani *limited* au dhima ambayo haina ukomo. Na hapa Mhe. Spika, ni muhimu kwa watu kujua kwamba unapoingia katika kampuni ikawa na *limited liability* basi lazima tujuwe kwamba chochote kile ambacho wewe umekifanya kwamba ndio *limited liability* yako, kampuni inapofika wakati wa kufunguwa kwa mfano au *wind up* wewe uliechukua dhima basi utawajibika kulipa kima kile ambacho umekikubali.

Na bahati nzuri hapa labda niseme mifano ambayo imetokea karibuni ofisini kwetu, kuna watu wanataka kuanzisha kampuni sasa baada ya kunzisha kampuni wakampa Mzanzibari asilimia 51 dhima yake yaani *limited company* ambayo yeye atachukua 51% *liability*. Yule Mzanzibari akafurahi kwamba wale watu wamempa asilimia 51, kwa hivyo, akipata faida atapata faida kubwa kushinda wale waliokuja

kuanzisha kampuni. Ukiliona hivi hivi linafurahisha lakini lina athari yake, wale wanaweza wakafanya manyanga mbali mbali, baadae ile kampuni ikafilisika, ikishakufilisika wewe uliepewa asilimia 51 itabidi lazima kisheria uzilipe.

Sasa uutizame uwezo wako je unaweza kuchukua dhima hiyo usidanganyike kuambiwa asilimia 51 si lazima wewe kwanza ulipe hizi fedha wewe tuendelee na kampuni baadae wanaweza wakafanya mambo ambayo yakahasidi kampuni, na ukalazimika sasa kisheria kulipa asilimia 51 wakati wao wameshaondoka au wameshakimbia. Sasa hilo waheshimiwa, wananchi naomba wajue kwamba tunapoingia katika utaratibu huu wa makampuni lazima tupate elimu nzuri ya namna gani tunaingia katika kampuni, kama kampuni zile ni *limited* au si *limited.*

Lakini kuna suala jengine ambalo limezungumzwa katika suala hili hili la *limited company* ni kwamba kama ni jina la kiswahili kwa mfano, uzalishaji wa mboga mboga jee unaweza ukandika *limited*? Mimi ninafikiri unaweza ukaandika uzalishaji wa mboga mboga wa Kichungwani *limited,* au kama hutaki *limited* utatumia lile neno la kiswahili lenye maana ya *limited.* Kwa hivyo haina matatizo kuandika Kiswahili ukasema uzalishaji wa mboga mboga wa Kichungwani *limited* ni sawasawa, inaonesha tu *liability* hiyo inakuwa ni *limited*.

Lakini Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa ni kwamba katika kifungu cha 26 nimesema kwamba kampuni inapoundwa ni lazima kuandaliwe nyaraka za aina mbili, ambazo ni Katiba ya kampuni yaani *memorundum of association* na kanuni za kampuni yaani *articles of association*. Hata hivyo, rasimu hii ya kampuni ambayo tumeileta ya sheria imeambatanishwa na orodha yaani kuna *schedule* kule nyuma tumeambatanisha ambayo ina kanuni za kampuni ambayo kampuni yenye hisa inaweza kuamua ama kutengeneza kanuni zake wanazokubaliana wao wenyewe au kama hawataki wanaweza wakatumia orodha ile ile ambayo tumeambatanisha. Kwa maana hiyo basi ndio maana tukasema zile kanuni kama zipo ikiwa hazipo ina maana kwamba kampuni ile itatumia zile zile ambazo zimefanywa katika *schedule* ya sheria ambayo tumeiambatanisha.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 21 kifungu hiki kina vijifungu 4 tukitizama mswada huu tumeweka vifungu 4 pale vijifungu vidogo. Vifungu 4 hivi, vitatu vya kwanza vinataja makosa yale mambo ambayo yamewekwa na tumesema kwamba adhabu ya makosa hayo yametajwa katika kifungu cha 4 yaani 21 *sub section* 4 kinachosema kwamba mtu atakaetenda kosa chini ya kifungu cha 1, cha 2, au cha 3 na iwapo mtu huyo ni kampuni, ofisa yeyote wa kampuni ambayo imekiuka masharti hayo atastahiki kutozwa faini na kwa kuendelea kukiuka anastahili

kutozwa faini ya ukiukwaji. Kwa hivyo, kifungu cha 21(4) ndicho ambacho kimeelezea adhabu ya makosa haya.

Na jengine ambalo Mhe. Spika, nilikuwa nataka kulizungumza la ujumla ni tofauti ya kampuni ya umma na kampuni ya binafsi. Kwa ufupi kampuni binafsi inajulikana kama kampuni za kifamilia ni kampuni zinazomilikiwa na watu wenye uhusiano maalumu kama baba vile, mama, watoto, ndugu na uhusiano mwengine wowote wa karibu. Kampuni hizi haziruhusiwi kuialika umma kununua hisa zake. Uhaulishaji wa hisa pia unafanywa kwa watu maalumu kwa ridhaa za wajumbe wa kampuni husika. Aidha katika kampuni hii ya binafsi idadi ya wajumbe mara nyingi huwa haizidi watu 50.

Lakini kwa upande mwengine ni vyema tu tufahamu kwamba kampuni za umma si kampuni za serikali (*Public Companies)*, lakini mtu yeyote anaweza kuwa mjumbe wa kampuni na hakuhitaji uhusiano maalumu baina ya wajumbe wa kampuni na wajumbe waliomo katika kampuni ile. Hisa za kampuni hii zinaweza kuhaulishwa kwa mtu yoyote na hakuna idadi maalumu ya wajumbe ambao wanaweza wakawemo katika kampuni inayohusika. Kwa hivyo, hii ndio tofauti kubwa na muhimu baina ya kampuni za binafsi na kampuni za *public*.

Mhe. Spika, baada ya hapo Mhe. Ussi yaani Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria yeye alitoa maoni yake pamoja na marekebisho ambaye ninamshukuru pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria tulikaa pamoja na tukayazingatia na tukakubaliana kwamba marekebisho yale ni muhimu ili kuweza kufanya sheria yetu kwa ni nzuri zaidi. Kwa hivyo mapendekezo yao tumeyakubali na tutayaingiza katika marekebisho ya mswada huu.

Lakini la pili Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Mohammed na yeye alizungumzia kuhusu kifungu cha 20 na nimeshakizungumzia kuhusu utaratibu wa majina namna gani Mrajis anaweza akabadilisha jina na niligusia hasa hapa katika yale majina ambayo yana mis-*lead*, yeye amesema *panasonic* kumbe si *panasonic* au amesema *panesonic* kumbe si *panesonic*. Sasa hayo ni mambo ambayo Mrajis awe na uwezo wa kuweza kubadilisha mambo kama haya.

Kuna suala jengine ambalo lilizungumzwa katika kifungu cha 4 kusema kwamba hizi *memorandum*, kwa nini tukasema kwamba ziwe za kingereza au za Kiswahili au pamoja na kanuni. Ni vizuri kusema hivyo kwa sababu makampuni yanayokuwa *registered* hapa si makampuni ya Wazanzibari tu ni makampuni ya nje, watu wengine ni wa nje kwa hivyo tusiweke kwamba lazima iwe kwa

kiswahili inaweza ikawapa uzito wale ambao ni watu wa nje na wanataka ku-*register* kampuni katika Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Amina yeye tunamshukuru alitoa mapendekezo yake ambayo ni mazuri na ukitizama hii sheria baadhi ya mapendekezo yake tumeya-*include* katika rasimu hii kwa hivyo nakubaliana naye na mawazo yake ambayo ameyazungumza.

Mhe. Fatma Mbarouk na yeye amezungumzia sana kuhusu *company limited by shares* na *company unlimited by shares* na tumesema kwamba *company limited by shares* ni kampuni ambazo hizi zina ukomo wa ile share. Kwa hivyo ukisema kwa mfano share holder mule ana 20% kwa hivyo likitokea lolote lile kwa hivyo yule mwenye asilimia ishirini itabidi alipe katika kiwango hicho cha asilimia ishirini.

Na pale ambapo zinalipwa zile tena kuna matatizo yale ambayo fedha ambazo ni zaidi ya pale hizo kwa kweli wale watu ambao wamepata athari wanaweza wakapata matatizo kwa sababu kwa mujibu wa sheria hii ya kampuni ni kwamba wale ambao wana *shares* watalipa katika kiwango kile cha *shares*. Na hapa ndio muhimu wa serikali kwa mfano na hata watu binafsi wajue utaratibu wa kuingia katika ubia wa kampuni hizi.

Kwa mfano ikiwa serikali unaingia katika ubia wa kampuni na kampuni ile wameshasema kwamba wao *liability* yao kwa mfano ni milioni hamsini, sasa mkafanya mkataba na shughuli ambazo pengine zina-*cost* kiasi milioni mia mbili, kwa hivyo linapotokea jambo lolote lile ile kampuni tumeshakubaliana, wao watalipa kwa kiwango kile cha milioni hamsini kwa hivyo ujue hayo tokea mapema. Kwa hivyo ni vizuri kuyajua haya ili unapoingia katika mikataba ya kampuni kama hizi ujue dhima na ujue kwamba likitokea lolote kiwango gani ambacho unaweza ukalipwa.

Mhe. Farida Amour Mohammed alizungumzia utaratibu wa kusajiliwa na akazungumzia sana suala la *inspection,* suala la ukaguzi. Napenda nimfahamishe tu kwamba kwa mujibu wa rasimu hii kuanzia kifungu cha 255 mpaka 258 pale imetajwa wazi, masuala ya *inspection* na katika vifungu hivi ni kwamba wahusika au Ofisi yetu itakuwa na utaratibu maalumu wa kuweka *inspectors* ambao wataweza kupitia baadhi ya mambo haya yanayohusiana na ukaguzi wa kampuni.

Mhe. Mshimba alizungumzia kuhusu semina za Wilayani ili watu waelimishwe, nakubaliana nae kwamba ni kweli kuna haja ya kuelimishana na hiyo ninafikiri kwa kushirikiana na wadau na Wawakilishi na watu wengine kwa ujumla tutafanya kazi hiyo ili tuweze kuelimishana. Kwa sababu kwa Wizara yangu peke yake hilo

ni suala kubwa na tusingeliweza kulifanya lote lakini kwa mashirikiano yenu ninaamini tunaweza tukakubaliana namna gani tuwaelimishe wananchi wetu ili waweze kupata taaluma zaidi ya masuala haya.

Hapa Mhe. Spika, labda nielezee tena zaidi kwamba tofauti kubwa iliyopo ni pale ambapo sisi tunatoa *registration* ya kampuni. Kutoa *registration* ya kampuni haihusiani kabisa na kwamba tumeshatoa idhini ya kuanzishwa kwa baadhi ya biashara zinazohusika, lazima upate kibali kutokana na taasisi inayohusika. Nilisema hapo mwanzo tunapokupa *registration* ya kampuni yako katika uvuvi kwa mfano kwa hivyo unapotaka kuanzisha zile shughuli za uvuvi lazima uende katika Wizara inayohsika ili Wizara inayohusika ikupe urataribu mzima, ikupe maelekezo, wanataka uvuvi namna gani, wanataka vyombo vya aina gani na kila kitu na hiyo bila shaka itabidi ushirikiane na ZIPA ili na watoe mapendekezo yao pamoja na utaratibu wao.

Kwa hivyo, sisi tunatoa *registration* ya kampuni lakini leseni ya ufanyaji kazi itakuwa ni taasisi nyengine na hapa labda niseme tu kwamba Mhe. Mshimba alizungumzia suala zima la mabadiliko ya kampuni. Kwa hivyo kampuni moja inaweza ikauzwa kwa watu wengine, sasa hii ni kweli unaweza ukawa na kampuni X lakini baada ya muda ukaiuza ikawa sasa ina jina Y na baada ya muda ikauzwa ikawa na jina Z.

Unapofanya hivyo pia kuna taasisi ambazo zinahusika, kwa mfano Wizara ya Fedha halafu kuna sheria ile ya ZIPA ambayo inataka pengine unapoanzisha kampuni kuna miaka 5 ya *grass period*, sasa jee, ukiiuza kwa kampuni nyengine *grass period* ile inaendelea au haiendelei, sisi wajibu wetu ni kuirejesha tu ile kampuni. Mambo mengine yoyote yanayohusiana na hizo kodi na mambo mengine ya *tax* na nini hayo ni Wizara ambazo zinahusika na mambo ambayo yanahusiana na hayo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba kuna suala la *inspection* ambalo Mhe. Mshimba na yeye alilizungumza katika kifungu 255 mpaka 258 lakini pia alizungumzia kifungu cha 256, kifungu 256 kimetaja adhabu lakini adhabu hizi zimewekwa katika jadueli nambari 2 na jadweli nambari 2 ina mambo mengi ambayo yamesema kwamba mtu akikosa au hakufanya kitu hiki kwa hivyo atapata adhabu hii, huku wamesema kuna daraja, kuna daraja A, daraja B, daraja C. Kwa hivyo, daraja A wamesema ni adhabu kiasi kadhaa, daraja B kiasi kadhaa hivyo hivyo kuendelea mpaka daraja C. Kwa hivyo, adhabu zote zimewekwa katika jadueli hiyo na kwa maana hiyo kifungu cha 21 pia kimeeleza adhabu yake ambao ukitizama kifungu cha 21(4) kimeweka vizuri na vifungu vyengine ambavyo vimo

katika sheria hii imeelezea kwamba kwa kosa hili basi adhabu yake iko katika jadueli namba 2 na itakuwa katika daraja A au daraja B au daraja C.

Mhe. Subeit alizungumzia suala la hisa, suala la hisa ni kweli lazima hisa ziwemo katika utaratibu ule mzima wa mkataba na ndio maana tukasema katika yale ambayo yapo, kuna *articles of association* na *memorundum of association.* Sasa zile ni kama mkataba wa ile kampuni na mule ndio inamotajwa zile hisa na kila mtu imetajwa mule hisa yenyewe. Kwa hivyo pale ambapo mnakubaliana lazima kila mtu aandike au akubali kwamba hisa zake ni zile ambazo zimeandikwa katika mkataba ule. Pia alizungumzia habari ya kampuni binafsi, ninafikiri kampuni binafsi nimeielezea na tofauti baina ya kampuni binafsi na kampuni ya *public*.

Mhe. Hamza yeye alizungumzia zaidi kuhusu utaratibu wa kuelimishana nakubaliana nae lakini kwa misingi hiyo, Wizara yetu itakuwa haina uwezo wa peke yake kupita Zanzibar yote kuelimishana. Kwa hivyo ninakubaliana nae kwamba tutashirikiana na wahusika wadau ili tuweze kujua kuweka utaratibu wa namna gani tunaweza tukaelimishana kwa faida ya wananchi wetu.

Na ilizungumzwa kwamba makampuni ni lazima yaweke utaratibu wa kutoa mikataba. Hapa napenda niseme tu kwamba kwa mujibu wa sheria hii kifungu cha 186 kimesema tu kwamba Wakurugenzi watazingatia maslahi ya wafanyakazi wao, hakikusema waziwazi kama alivyosema Mhe. Hamza. Lakini hii haikusema hivyo kwa sababu moja, kwa sababu maslahi ya wafanyakazi yako katika Wizara nyengine Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma ambao wao ndio wanao-*monitor* wafanyakazi wote, lazima kuwe na mikataba, lazima kuwe na utaratibu fulani.

Kwa hivyo, sisi hapa tumewafunga wao kwamba lazima wazingatie maslahi hayo, lakini maslahi hayo yatakuweko katika Wizara ya Kazi ambao wataweka mikataba kwa mujibu wa utaratibu wao ambao wanahisi unaweza ukasaidia wafanyakazi hao. Kwa hivyo, nakubaliana naye Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba wafanyakazi lazima wazingatiwe lakini kwa misingi hiyo, kwa misingi ya kuweka mikataba lakini mikataba ya wafanyakazi iko katika sheria ya wafanyakazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma yeye namshukuru kwa maelezo yake aliyoyatoa, lakini alizungumzia kampuni hizi kwa mfano Kampuni ya Maziwa, Kampuni ya Biashara, Kampuni ya Biashara Chakavu zile za vitu vichakavu. Sasa zile napenda niseme kama nilivyosema mwanzo, kwamba sisi hatuhusiani sana na masuala haya, wewe unapokuja kujisajili katika ofisi yetu kwamba unaanzisha kampuni sisi tunakubali tunakupa *registration*, lakini *registration* tunayokupa ni kuanzisha

kampuni sasa unapoanzisha kampuni inategemea kampuni gani. Kwa mfano ni biashara ya vitu chakavu kwa hivyo pale lazima wende katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Biashara watakuwa na utaratibu wao, watakuwa wana mambo yao chungunzima ya kufuata ili kuanzisha utaratibu huo.

Baada ya kukubaliana utaratibu baina ya wewe na Wizara ya Biashara ndio pale Wizara ya Biashara watakupa kibali au leseni ya kuanzisha hiyo biashara chakavu. Kwa hivyo, hapa kuna mambo mawili ambayo lazima tuyakamilishe. Ingawa kwa utaratibu ambao hivi sasa tunajaribu kuuandaa ni kwamba mfanyabiashara yule anayetaka kuanzisha kampuni halafu akaanzisha biashara ya kitu fulani zote tunataka ziwe katika sehemu moja (*one stop center)*, unakuja pale una-*register* kampuni yako pale pale unakwenda dirisha jengine unaanzisha kampuni yako kwa masharti ambayo unakubaliwa na mambo kama hayo, lakini hii ni *process* ambayo tunaianza hivi sasa na tunatizama utaratibu gani ambao tuuchukue ili tuweze kufikisha hayo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mchangiaji mwengine ni Mhe. Mgeni Hassan Juma, yeye alikuwa na mambo mawili muhimu. La kwanza alizungumzia sana suala la *subsidiary Company*. Katika utaratibu wa kuanzisha makampuni, kampuni inaweza ikaanzishwa hapa au mfanyabiashara anaweza akaanzisha kampuni nchi za nje. Sasa akianzisha kampuni nchi za nje anaweza akaja akafungua *subsidiary company* hapa ambayo imeshaanzishwa kule, akianzisha *subsidiary* hapa lazima afuate utaratibu ambao tumeuweka, aje azi-*register* tena zile *articles* na *memorandum* ili tuzielewe, lakini pili lazima kuwe na mkaazi wa kampuni ile, mtu ambaye anakaa hapa. Kwa sababu moja tu, kwamba linapotokea tatizo lolote au tunapotaka kuwapa *notice*, au tunapotaka kuwaita kuwe kuna mtu ambaye yupo katika maeneo yetu tuweze kumwita, tuweze kumwambia kwamba kuna tatizo hili na hili.

Kwa hivyo, ndio tukasema kuwa inapoanzishwa *subsidiary company* lazima kuwe na mkaazi na mkaazi huyu si lazima awe ni Mzanzibari anaweza akawa ni mtu yeyote ambaye keshapata vibali vinavyohusika. Kwa hiyo atakuwepo hapa na tunaweza tukamwita kwa kumpa *directives* kuhusiana na kampuni yake au kumwambia kwamba kampuni yake ina matatizo haya na haya yarekebishwe na utaratibu kama huo.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hili ni jambo la kawaida na ningelipenda tu niseme kwamba, utaratibu wa kampuni takribani ni utaratibu unaotumika sawa sawa karibu nchi nyingi za ulimwengu. Hivyo mambo yetu yote ambayo tunayafanya lazima yashabihiane na utaratubu ambao upo Tanganyika, Kenya, Uganda, Malawi na nchi nyengine na tukifanya hivyo ndio tunazidi kuhamasisha wale waanzishaji

kampuni kuja katika maeneo yetu Zanzibar na waweze kuanzisha kampuni. Lakini tukiweka vikwazo vikubwa watu hawatoanzisha kampuni hapa wataona bora waanzishe pahala pengine na ndio maana hiyo tumejitahidi hivi sasa unapotaka kuanzisha kampuni yako basi *mostly* tunachukua siku mbili lakini pengine hazifiki sasa kwa kuanzisha kampuni yako, kama utajaribu kufuata utaratibu wote ambao umewekwa katika kanuni zetu na utaratibu wetu.

Kwa mfano ukija leo *by tomorrow* kampuni yako itakuwa imeshakuwa *registered* na tutajaribu kufanya zaidi hivi ili tuweze kuwakaribia wenzetu. Wenzetu hivi sasa ku-*register* kampuni ni masaa tu, lakini bado tunajaribu kufanya utaratibu mzuri ili mtu anapotaka ku-*register* kampuni basi kwa masaa kidogo tu au kwa siku moja, lakini hivi sasa haizidi siku mbili. Kwa hivyo, ukija leo, kesho tunahakikisha kwamba kampuni yako imeshakuwa *registered*, labda tuwe na matatizo ambapo matatizo yale tutakueleza na utayarekebisha ukishakuyarekebisha basi tunai-*register*.

La pili ambalo ni la mwisho Mhe. Mgeni Hassan alizungumzia huu utaratibu wa waziri ataweza au anaweza kutunga kanuni, waziri anaweza kufanya hivi, waziri anaweza kuteuwa. Huu Mhe. Spika, ni utaratibu wa kawaida katika sheria, kwa sababu unaposema kwamba waziri atateuwa au waziri atatunga kisheria analazimika sasa atunge na pengine patakuwa hapana haja ya kufanya hivyo kwa wakati huo. Sasa sisi tunachukulia kwamba waziri yoyote atakuwa ni waziri ambaye anajua jukumu lake na pale ambapo itahitajika kutunga basi atafanya hivyo, lakini ukisema waziri atatunga kanuni kwa hivyo *it means* hiyo ni *compulsory*, ni lazima atunge ndio ziweze kutekelezeka.

Kwa hivyo, uandishi mzuri wa kisheria ni kwamba tusimfunge yule waziri tumpe nafasi, pale ambapo inahitajika basi anaweza akatunga kanuni au anaweza akafanya mambo mengine ambayo yanakubalika.

Mwisho Mhe. Spika, kama nilivyosema Mhe. Salma Mohammed Ali alileta maelezo yake kwa maandishi na moja nafikiri nimelizungumza na la pili pia nilipokuwa nikimjibu Bi Mgeni, naye pia ndio nimeshamjibu. Kwa sababu alisema kwamba suala la waziri anaweza.

Lakini suala jengine ambalo alilizungumza Mhe. Salma Mohammed alisema kwamba kifungu cha 256…

Mhe. Spika: Mhe. Waziri anakaribia kufikia mwisho wa majumuisho yake, hivyo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe sasa wabakie ndani tumalize kazi hii. Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Alisema kifungu cha 256 faini yake ni ndogo na mule tumesema shilingi elfu 40, 20, 15, hizi si faini ndogo katika masuala kama haya. Kwa sababu ni faini kwa mfano hukupeleka fomu moja tu ambayo inatakiwa upeleke, hatuwezi kuweka faini shilingi milioni tano au mbili hizi kampuni tutazifukuza na hii utaona katika utaratibu wetu takribani faini hizi zinalingana na wenzetu. Kwa hivyo, kila tukiweka faini ambazo zinalingana ndio hao waanzishaji wa kampuni hatutowapa njia ya kuondoka nchi yetu na wao wataweza kuja na kupandikiza makampuni yao.

La pili ambalo amelizungumza ni lile la uandikishaji wa kampuni kwa Kiswahili. Tunaweza kufanya hivyo na la tatu ni kwamba sheria ipange kuondoa urasimu. Tutajitahidi kufanya hivyo na ndio maana nikasema kwamba kwa hivi sasa unapoanzisha kampuni basi tunahakikisha kwamba kwa siku mbili kama utakuja leo basi kesho *registration* utaipata, labda kuwe na matatizo ambayo lazima yarekebishwe tunashirikiana, lakini tumejitahidi ambapo hivi sasa ni siku mbili tu na *Inshaallah* baadae tunaweza tukapunguza kutoka siku mbili.

La mwisho alilozungumza ni kwamba nchi yetu itegemee zaidi kampuni za wazawa kuliko kampuni za nje. Hii ni sawa lakini ni uhamasishaji, uhamasishaji wa watu wetu na hasa wale ambao wana uwezo wa kuanzisha kampuni. Kwa hivyo, wao wakiona kwamba hapa waanzisha wa kampuni wanaweza wakafaidika zaidi basi tungeliomba sana wafanye hivyo, lakini hii inakwenda sambamba na mambo mengine ya uanzishwaji wa Kampuni. Sheria za uanzishwaji wa kampuni ziwe ni nzuri, sheria za *ZIPA* ziwe zina vivutio vizuri na sheria nyengine za fedha utoaji wa kodi, malipo ya kodi ya *tax* zote zikiwa ni nzuri basi hapo uanzishaji wa kampuni wa ndani na wa nje watu watavutika sana na kuanzishwa kampuni katika maeneo yetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, napenda sana niseme kwamba, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa maelekezo yao na miongozo yao ambayo wametupa tutayafanyia kazi na *Inshaaallah* ikipita sheria hii tutajitahidi kuiharakisha ili iweze kuanza kazi ili iweze kuanza kazi kwa haraka na watu waweze kuwa na muamko mpya katika usajili wa makampuni.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba sasa kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu ndivyo tunavyofanya Mhe. Spika, lakini kutokana na sheria hii kuwa ni kubwa sana ina vifungukaribu 270. Kwa hivyo, naomba nitoe hoja ya pili kwamba badala ya kupitia kifungu baada ya kifungu kwa mujibu wa Kanuni 87(1)(2) za Kanuni za Baraza la Wawakilishi sasa naomba nitumie kanuni ya 156 ili tutengue utaratibu huu wa kwamba baada ya kupitia kifungu baada ya kifungu tupitie *chapter* baada ya *chapter*. Kwa mfano sheria hii ina *chapter* 11 sasa naomba tutumie utaratibu huo wa kuita *chapter* au sura ya kwanza ambayo ina vifungu kwa mfano vitano au sita.

Sasa kama mtu ana hoja katika vifungu vile ata-*raise* hoja yake kwa kupitia kifungu kile tukimaliza tunakwenda *chapter* ya pili au sura ya pili ambayo ina vifungu pengine 20 kama kuna mtu ana hoja katika sura ile ata-*raise issue* yake ili tuweze kumaliza kwa muda mdogo zaidi kuliko kupitia kifungu baada ya kifungu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja mbili, ya kwanza kwamba Baraza likae katika Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu na ya pili Mswada huu tuupitie kwa sura hadi sura badala ya kifungu kwa kifungu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna maombi mawili hayo, moja ni taarifa kwamba Kamati sasa ikae, lakini kabla ya kukaa kamati hoja imetolewa kwamba *volume* hii ni kubwa, kwa hivyo tuwe tunapitisha kwa humu nadhani inaitwa sehemu kwa sehemu. Sasa tuta *pause* pale tunapouliza sehemu kuangalia kama kuna Mjumbe ana hoja ya jambo lolote katika eneo hilo basi aseme kabla hatujenda kwenye sehemu nyengine, kama hakunyanyuka mtu maana yake sehemu hiyo kwa ujumla wake vifungu vyake ndio vimeshapitishwa. Sasa niwahoji

Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunajaribu ku *thought-out* ili tuwaelekeze Waheshimiwa Wajumbe zile sehemu kwa sehemu ni ukurasa gani huo, mana hii hoja tuliyopitisha ilikuwa hatukuiandaa. Kwa hivyo, tusione kimya hapa hakuna kazi nyengine isipokuwa ku-*thought-out* hiyo.

Waheshimiwa tutakwenda taratibu ili tunapotaja ukurasa Waheshimiwa Wajumbe tuweze kufuatilia kwa karibu, kwa sababu hizo sehemu kurasa zake ziko mbali mbali kwa mujibu wa vifungu vilivyomo kwa kila sehemu. Kwa hivyo, tutakuwa tunakwenda taratibu ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kufuatilia kwa karibu.

Mswada wa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2013

Sehemu ya Kwanza	Utangilizi pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Pili	Usajili wa Kampuni na Masuala yanayohusiana nayo pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Tatu	Uwezo wa Kampuni na Masuala yanayohusiana nayo pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Nne	Mtaji wa Hisa na Dhamana pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Tano	Uandikishaji wa Malipo pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Sita	Usimamizi na Utawala pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Saba	Ufungaji wa Kampuni kwa Hiari ya Wajumbe pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Nane	Kampuni zilizoandikishwa nje ya Zanzibar pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Tisa	Masharti ya jumla kuhusu usajili pamoja na marekebisho yake.
Sehemu ya Kumi	Masharti mengineyo kuhusiana na Kampuni za Benki na Bima na Jumuiya nyengine, Ubia na Kampuni zilizosajiliwa pamoja na marekebisho yake.
Sehemu Kumi na moja	Mambo ya jumla pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali mswada huo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: WAheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana na mswada pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kampuni ya mwaka 2013 sasa usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huo katika kusomwa kwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Ahsante sana, naona leo shughuli hii imetumika mpango maalumu, mbinu maalumu za Jimbo la Mgogoni, lakini zimesaidia sana katika kufanikisha shughuli hii kwa wakati. Tunaendelea.

17/10/2013

Mswada wa Sheria ya Biashara Zanzibar, 2013

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe shughuli ya Mswada huu kama mtakumbuka ilikuwa Mswada umerejeshwa kwenye kamati ili kusawazisha baadhi ya mambo. Kwa hiyo, kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri naomba nimkaribishe Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maelezo mafupi juu ya suala zima la ombi la kuakhirisha kwa muda kuendelea na mswada ule kutokana na mambo ya hapa na pale ambayo yalijitokeza.

Kwanza Mhe. Spika, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Baraza hili Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ndie aliekuwa akiongoza kikao kile jioni ya siku ile.

Pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe waliokubaliana na hoja ya kumuomba Mhe. Kaimu Waziri kwa kuakhirisha mjadala ule ili kamati yangu ipate nafasi ya kukaa na wizara na kufanya baadhi ya masahihisho yaliokuwa yamejitokeza ndani ya mswada ule.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yale nilipata masuala mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe na baadhi ya watu mbali mbali ambao waliniuliza ni kwa nini mswada ule niliomba uakhirishwe kwa muda na ilhali kwamba hotuba yako ilisomwa na haikuelezea juu ya hoja hiyo. Lakini pili kulikuwa na marekebisho ambayo wewe kama Mwenyekiti uliweka saini.

Mhe. Spika, Ni kweli walikuwa wana sababu ya kuuliza hilo na kutaka kufahamu na kwa sababu si jambo la kawaida na si jambo ambalo lililowahi kutokea katika chombo hichi. Kwa hivyo, walikuwa na wajibu wa kutaka kufahamu.

Lakini Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba kwa mujibu wa kanuni zetu mswada kabla ya kuwasilishwa hapa Baraza unatakiwa uwasilishwe katika kamati inayohusika ili kamati ile ipate fursa ya kujaa pamoja na wizara ambayo inayohusika na huo mswada wakiwemo pamoja na Wanasheria wa Serikali na Wanasheria wa Baraza letu ili kuupitia upya na kuuangalia na kujiridhisha juu ya madhumuni ya mswada ule na mambo mengine yanayohusiana na mswada ule ili tuone kwamba mswada ule au sheria itakayotungwa kutokana na mswada ule basi inakuwa sheria inayozingatia maslahi ya nchi na wananchi kwa ujumla. Na kwa

sababu chombo hichi mara zote wakati kinapotunga sheria huwa kinazingatia masuala hayo na kuhakikisha kwamba sheria ile inatekelezeka.

Lakini kilichojitokeza Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tukiupitia mswada ule kwa awali tuligundua mambo kadhaa ambayo ni makubwa.

Kwanza tuligundua kwamba kulikuwa na tafrisi tafauti kati ya mswada ule wa kiengereza na ule wa kiswahili.

Pili, tuligundua kwamba hata vile vifungu vilivyotafsiriwa kwa kiswahili vilikuwa havikueleza ile dhana kamili ya mswada ule iliyokusudiwa. Lakini hata makosa ya uchapaji nayo yalijitokeza mengi sana. Jambo ambalo lilitusababisha tuanze sasa kuandika upya mswada ule. Tulifanya kazi hiyo ambayo kwa kweli haikuwa yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Kaimu Waziri kwa wakati ule na Naibu Waziri pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambao tulikuwa nao tulishirikiana kwa pamoja katika kuona kwamba mswada ule unakuwa ni bora na unazingatia yale matarajio ambayo yamekusudiwa.

Hili Mhe. Spika, tulikubaliana kwa pamoja na pia tulikubaliana kwamba baada ya marekebisho hayo basi mswada ule wende ukachapishwe upya kwa sababu huwezi kuleta mswada ambao una marekebisho yaliokuwa mengi kuliko ule mswada wenyewe. Kwa hivyo, hilo Mhe. Spika, tulikubaliana.

Sasa baada ya kuruhusu mswada ule ukachapishwe upya kwanza mswada ule ulichelewa kufika katika Baraza lako. Mswada ambao ulikuwa unatakiwa ujadiliwe siku ya Ijumaa asubuhi ulifika hapa Barazani mchana siku ya Alhamis na katibu wangu akanipigia simu akanambia mswada ule umefika sasa hivi tunajaribu kuupitia tuone kama kuna mapungufu. Mbali ya yale marekebisho ambayo tulikubaliana kwamba yarekebishwe lakini yakawepo mengi ambayo yamejitokeza tena.

Lakini Mhe. Spika, kutoka na kamati yako haikupata nafasi ya kuupitia upya mswada ule kwa sababu muda ulikuwa haupo. Umefika Alhamis na Ijumaa tunaujadili. Kwa kuwa hatukupata nafasi ya kuupitia upya tungetemea kwamba yale marekebisho yote ambayo tulikubaliana basi yangezingatiwa. Lakini kwa bahati mbaya sana mengi ya marekebisho ambayo tuliyokubaliana hayakuzingatiwa wakati wa uchapi wa mswada ule ni baadhi tu.

Kwa hivyo, kutokana na hali hiyo tulilazimika au nililazimika kama Mwenyekiti wa kamati ile kuomba tuakhirishe mjadala ule ili kamati yangu ipate nafasi sasa ya

kwenda kupitia upya na wizara pamoja na wanasheria na kuona yale mapungufu ambayo yamejitokeza ambayo ni mengi tunakubaliana kwa pamoja na hatimae mapungufu yale yawasilishwe hapa katika chombo chako.

Nashukuru sana namshukuru sana Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu ambae tumeshirikiana kwa pamoja na kutengeneza *schedule of amendment* ambayo sasa hivi nadhani imegaiwa. *Schedule of amendment* hii tumekubaliana kwamba sasa ni sahihi yale yote ambayo yalioachwa ambayo tulikubaliana yamezingatiwa. Lakini pia yamezingatiwa na yale marekebisho pia imepata nafasi ya kuzingatia yale mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe na mengine mengi yamezingatiwa na nadhani mmeiona *schedule of amendment* ilivyosheheni mambo.

Lakini moja kubwa ambalo liliachwa ambalo nalo lilinilazimisha ni juu ya makubaliano yetu ya kuweka katika sheria ile jeduweli ya adhabu ambayo nayo imezingatiwa. Adhabu ambazo kwenye kamati tulikubaliana kwamba ziwekwe sawa na kwa sababu zilikuwa hazianishi mfanyabiashara mdogo wa kati na yule mkubwa juu ya adhabu ya kosa moja ambalo linatendekea.

Kwa hivyo, nashukuru kwenye *schedule of amendment* juzi tumekubaliana na hayo limezingatiwa. Kwa hivyo, sasa katika hatua hii kamati yangu imeridhishwa na *schedule* hii na Waheshimiwa Wajumbe mtapata nafasi ya kuipitia kama kuna marekebisho mengine ya ziada, kwa sababu hatuwezi kuyamaliza yote mtaeleza. Lakini kwa kamati sasa hatuna wasi wasi na *schedule of amendment* ambayo Mhe. Waziri ataiwasilisha hivi punde ili sasa sheria yetu iwe imekamilika na iwe imezingatia yale matakwa ya kamati na matakwa ya Baraza zima.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tujadili sasa rasimu hii tuweke mengine ambayo tunahisi ni bora hatimae tupate sheria iliyokuwa bora.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ninachokifahamu ni kwamba mjadala ulimalizika na leo baada ya kutoa taarifa hii ya kamati basi tunakwenda katika majumuisho. Utaratibu Mhe. Hamza Hasssan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza na mimi kwa upande wangu nataka nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa umakini wake mkubwa hasa katika mswada ambao walihisi ulikuwa na marekebisho mengi ambayo walishauri wizara hawakuweza au yaliwapitikia hawakuweza kuyafanyia kazi.

Baada ya makubaliano yetu ya juzi Mhe. Spika, kwamba tuakhirishe ili kamati ikae tena ili kujaribu kuangalia yale mapungufu.

Mhe. Spika, huu mswada hivi sasa ninavyokwambia marekebisho haya yamoto. Yamoto maana yake ndio kwanza tumepewa baada ya hayo marekebisho baina ya kamati na wizara. Na mimi kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, mwezangu alisahau nilimuomba tu kwa kuwa mlikuwa mnahisi kuna marekebisho mengi hebu tualikeni na sisi alau tuje tusikilize katika kufanyiwa hayo marekebisho. Lakini kwa habati mbaya inaonesha walipitikiwa.

Sasa sikukusudia kwamba lazima nialikwe mimi. Lakini tatizo lililojitokeza Mhe. Mwenyekiti, mswada haya marekebisho ni mengi sana na tukisema tu kwamba msada huu ulikuwa tayari umeshajadiliwa sasa hivi aitwe Mhe. Waziri na hii *schedule of amendment* kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti hapa ni kubwa sana.

Sasa inawezekana na sisi kwa sababu kamati wameyaona baadhi. Lakini na sisi nafikiri tungepata muda vile vile wa kuyaona mengine ili sasa tunapokuja kuishauri wizara hii sheria ijekuwa sheria makini na kwa kuzingatia Mhe. Spika, sheria hii katika sheria ambayo inayowagusa Wazanzibari wengi ni sheria hii.

Katika masuala ya biashara Mhe. Spika, katika kila jimbo kuna wafanyabishara karibu robo ya wakaazi wa jimbo tafauti na hizi sheria nyengine nyepesi nyepesi tunazozipitia. Sasa hofu yangu tusije tukasema twende moja kwa moja bila na sisi kupata muda mzuri wa kuweza kuangalia kwa sababu pengine wao walipokaa kamati na wizara waliona hivyo. Lakini pengine sisi tungeliweza kuona zaidi.

Sasa nilikuwa naomba Mhe. Spika, utumie busara zako kwamba na sisi utupe muda kama kamati walivyopata muda wakakaa na wizara. Tupate muda mzuri ili sasa na kujaribu kuangalia vile vifungu ambavyo vilivyoletwa na waziri vilivyorekebishwa na vilivyorekebishwa tena na kamati ili tutakapotoa maoni yetu yaendane sambamba na huu mswada wenyewe.

Mhe. Spika, vyengine inaweza tukaja kupitisha hapa sheria ambayo baada ya muda mchache tukaja kuomba kufanya tena marekebisho. Sasa nilikuwa naomba tu kwa busara zako Mhe. Spika, mimi ningeliomba tu tupewe muda zaidi ili siku itakayofuata yaani kesho tuje kupata nafasi nzuri ya kuweza kuchangia vizuri. Kwa sababu sheria hii tulikuwa tuna hamu nayo sana kama tulivyosema kwamba ni sheria ambayo inagusa watu wengi sana.

Kwa heshima na taadhima Mhe. Spika, nilikuwa tu naomba upokee maoni yangu na naamini wenzangu watanikubalia kwa hoja hii. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Hii inaonesha maana yake ni kwamba mjadala ulikuwa haukumalizika. Sasa basi itabidi majadiliano yaendelee. Haya pendekezo Mhe. Ismail Jussa Ladhu .

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, bila ya kuyarejea yale ambayo tayari Wajumbe wawili wameyaeleza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Mhe. Mwakilishi wa Kwamtipura Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mimi nilikuwa nadhani ule utaratibu uliokuwa umeelezwa mwanzo tu ungezingatiwa kwa sababu kumeletwa *schedule of amendment* ya pili baada ya kurejeshwa kwenye kamati ungelimuomba na kumruhusu Mhe. Waziri akaiwasilisha hiyo sheria ya *schedule of amendment* ambayo wamekubaliana pamoja na kamati.

Halafu tukaakhirisha kikao ili kukapata nafasi ya kwenda kuitafakari na kesho tuitumie kwa mjadala Mhe. Spika.

Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma vifungu ambavyo tumeletewa ni vingi na tangu mwanzo ilikuwa inatukanganya kwa sababu kulikuwa na mswada wa mwanzo ukaletwa wa pili tukaletewa marekebisho ya kamati ya awali ambayo ilikuwa si kidogo ambayo tuliyapata siku ile ile ikabidi kuyapitia pamoja na mswada ule.

Lakini halafu mwenyekiti mwenyewe wa kamati akaona kuwa kuna marekebisho ambayo amependekeza hayakuwa yameingizwa katika mswada uliochapishwa upya.
Na sasa hivi Mhe. Spika, tumepata waraka huu ambao una kurasa 13 na baadae vile vile una kurasa nyengine tatu za vijalizo vya marekebisho ya jaduweli na kama ulivyesema umebadilisha mambo mengi ya msingi ikiwemo kuondoa mambo yale

ambayo yamelalamikiwa sana kwa mambo ya adhabu na tukapeleka kwenye mambo ya jaduweli.

Sasa nilikuwa nadhani kwamba ni muhimu Wajumbe tukapata nafasi nzuri ya kuyapatia kuyaoanisha na mswada ambayo tayari uligaiwa ili baadae kama alivyopendekeza Mwakilishi wa wananchi wa Kwamtipura tutakapopitisha sheria iwe imekaa vizuri na sote turidhike na *consciousness* yetu iwe *clear*. Kwamba mswada huu utakuwa umekidhi yale masharti ambayo tunadhani tunapaswa tuwe nayo na kuwa sheria nzuri baadae itakwenda kutumika na wananchi.

Ningeomba Mhe. Waziri angewasilisha *schedule* lakini baadae tupate fursa ya kina kwa sababu si dhani kama akipitisha tu pale tutakuwa na muda wa kutosha kuelewa na kuweza kuyachangia. Kwa sababu wengi wetu tulisita kuchangia ile siku wa mwisho. Kwa sababu tulikuwa tunapata matatizo haya ya kuchanganywa na mswada kuchapwa upya na marekebisho ambayo kamati ilikuwa imeyaleta mengi yalikuwa bado hayaoani.

Kwa hivyo, nilikuwa nadhani kwamba sasa vile vile tusirejee makosa yale tungemuomba Mhe. Waziri akawasilisha na baadae tukapata fursa kuyapitia kwa kina. Naomba kutoa mapendekezo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nimefahamu *concern* ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba haya marekebisho yaliyoletwa ni mengi na hakuna ubishi katika hilo. Lakini sasa taarifa niliyokuwa nimepata kwa Mhe. Mwenyekiti ilikuwa ni kwamba jambo hili michango imemalizika ndicho ambacho ameniarifu na *note* anayoniletea sasa hivi anakumbusha hayo hayo kwamba hakukuwa na wachangiaji wowote, michango imemalizika isipokuwa kuna hili ombi.

Lakini tuzingatie na ratiba yetu vile vile mimi sina pingamizi kuhusu hilo kumruhusu Mhe. Waziri awasilishe rasmi. Lakini sasa itabidi tuje jioni ili kesho sasa waziri aje afanye majumuisho.

Mhe. Waziri karibu kuwasilisha rasmi kile mlichokubaliana ndani ya kamati.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kufanya majumuisho ya Mswada wa Sheria ya Biashara Zanzibar namba 4 ya mwaka 1989 na kuanzisha sheria ya Biashara ya mwaka 2013 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao walioitoa na takribani Wajumbe 13 walichangia katika waraka huu hapo mwazo.

Vile vile, namshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Naibu Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko katika majumuisho haya nae alielezea mengi katika kufafanua masuala yenyewe.

Waliochangia mswada huu Mhe. Spika, ni Waheshimiwa 13 naomba niwataje wa ruhusa yako ...

Mhe. Spika: Mhe. Waziri nafikiri hatukufahamiana, wanachosema Waheshimiwa Wajumbe kwamba baada ya marekebisho haya mliyokubaliana katika kamati inaonekana bado kutakuwa na maelezo ila tu cha muhimu ni kukumbuka wale waliokwisha changia itakuwa basi.

Isipokuwa kama kuna wapya kutokana na marekebisho haya basi wachangie. Tunachozungumza hapa sasa wasilisha rasmi hichi ulichokifanya ndani ya kamati ili Wajumbe wachangie kama watakuwepo katika muda huu sawa. Lakini kama hawatakuwepo basi wapate huo muda kusoma ili jioni tuendelee na mjadala.

Lakini kimsingi mimi niliarifiwa kwamba michango ilikwishamalizika hicho ndicho nilichoarifiwa. Na kwamba kazi iliyobaki ilikuwa ni majumuisho baada ya jambo hili kwenda kwenye kamati ili kuondoa ile tafauti ambayo imeonekana katika kamati na wizara namna ilivyowasilisha.
Sasa mimi mtizamo wangu ulikuwa tunakuja hapa kufanya majumuisho ambayo Mwenyekiti ameshawasilisha. Hii ndio kazi iliyofanywa ndani ya kamati pamoja na Mhe. Waziri.

Ila sasa kumbe tunataka kufungua mjadala zaidi, tukifungua mjadala zaidi maana yake tupate Wajumbe wapya wale ambao watakuwa na maoni tofauti na yale ambayo yalielezwa hapo nyuma. Kwa sababu kanuni inaruhusu Mjumbe kutoa maelezo mara hii moja katika kuchangia mswada.

Sasa kama hivyo ndivyo basi wasilisha rasmi tufungue mjadala. Bahati mbaya sina zile kumbukumbu za wepi wamechangia na wepi hawajachangia. Lakini vyenginevyo Mwenyekiti anataka kunisaidia. Lakini ilikuwa hapa tunarejea katika majumuisho kwa kuona kwamba sasa zile tafauti ambazo zimeonekana zimerekebishwa kutokana na *schedule* hii.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tupe maelekezo.

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kutoa maelekezo kidogo ili kuweka haya mambo yetu sawa.

Mhe. Spika, kazi ambayo niliifanya juzi kwa niaba yako Wajumbe walichangia kwa mujibu wa taratibu ziliopo na Wajumbe walimaliza wale ambao wako hapo nafikiri ziko *paper* hapo mbele kuna jumla ya Wajumbe 10 na wa kumi na 11 alikuwa ni Mhe. Mwenyekiti mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti alikuja na hoja kwamba yale ambayo walikuwa wamekubaliana katika kamati hususan katika eneo la adhabu pale palikuwa na utata kwa sababu zile adhabu hazielekezi mwenye adhabu kubwa anachukuliwa hatua gani na yule mwenye kosa dogo anachukuliwa hatua gani. Kutokana na hoja yake hiyo Mwenyekiti ndio nilikubali kwamba waende wakakae baina ya kamati na waziri pamoja na wizara yake husika ili wakarekebishe yale matatizo ambayo yalikuwa yamejitokeza ili baadae baada ya kwisha kuwa Mwenyekiti mwenyewe ameridhika na yale mambo walikuwa wamekubaliana ndio waje hapa kwa ajili ya majumuisho.

Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma, amekuja na hoja nyengine amesema kwamba:

> "Pamoja na utaratibu ambao ulikuwa umewekwa kuna mambo ambayo mazito yamejitokeza"

Hili ni suala jengine ambalo pale mwanzo halikuwepo. Sasa naomba utumie busara zako katika kuona kwamba hili suala tunaliweka sawa katika utaratibu unaopaswa.

Lakini juzi tuliondokea kwamba ule utaratibu wa adhabu haukukaa vizuri na ndio maana tukatoa maelezo waende wakakae ili wakubaliane katika hilo. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika. Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma, hebu nikuulize hivi uliwahi kuchangia huko nyuma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, mimi sikuwahi kuchangia mswada huu na sikuwahi kuchangia kama alivyozungumza mwenzangu kutokana na ule mkanganyiko wa baadhi ya mambo.

Kawaida Mhe. Waziri anapoleta hoja yake baadae mwenyekiti akachangia ile ripoti yake. Kwa hiyo, sisi tunachangia mswada kwa kuangalia maeneo yote

mawili kuangalia mswada aliouleta Mhe. Waziri. Lakini vile vile kuangalia na maoni ya kamati. Kwa sababu pengine mswada ulikuwa unasema hivi lakini maoni ya kamati yalishauri vyenginevyo na mara nyingi tunakwenda samabamba hasa na maoni ya wenyeviti au maoni ya kamati yalivyopendekeza.

Sasa kama anavyosema Mhe. Mwenyekiti, juzi baada ya kuwasilishwa ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ambayo aliisoma Makamo wake na wachangiaji walichangia na sisi wengine tulibakia kunyamaza kimya maana yake unajua si uzuri kuzungumza kitu ambacho huna uhakika nacho. Na hili Baraza la Wawakilishi mkipitisha jambo linatakiwa liwe vizuri.

Sasa hii *schedule of amendment* alau ingelikuja kama alivyosema Mwenyekiti kwenye zile adhabu. Lakini haya marekebisho wamekwenda kuyafanya upya wamekwenda kukaa tena. Sasa ndio maana tukasema *at list* tukapata muda kidogo tukajaribu kuupitia tena ule mswada pamoja na haya marekebisho alau tukajua kile tunachokipitisha, tunakipitisha kitu gani.

Kwa sababu kama kuna marekebisho yamefanywa na sisi tulikuwa na haki ya kuweza kutoa maoni vile vile. Lakini sasa kwa muda huu mchache uliokuwepo kwa ghafla na kama nilivyosema haya marekebisho yameletwa hivi punde hatuhapata hata nafasi ya kuweza kuchungulia.

Kwa kweli ilikuwa si busara sana kuweza kupitisha kitu ambacho na sisi tutakuwa hatuna uhakika nacho. Ndio maana tukaomba busara zako Mhe. Spika, ilikuwa Mhe. Waziri awasilishe *schedule of amendment* halafu tuahirishe Baraza aidha tuje kesho kwa ajili ya kuuchangia. Kwa kuwa wamekwenda kufanya marekebisho haya marekebisho yalitakiwa yachangiwe.

Wajumbe waliochangia mwanzo walichangia kwa mujibu wa marekebisho yalivyofanywa na kamati. Lakini haya ni marekebisho mengine yamefanywa. Kwa hivyo, hata inawezekana kama Mjumbe aliwahi kuchangia lakini baadae kile alichokichangia alikikubali lakini baadae kile alichokichangia alichokikubali huku kimesharekebishwa. Sasa atakuwa amekubali nini?

Alikubali kitu ambacho kimesharekebishwa na sasa hivi kile alichokikubali kitakuwa sicho. Sasa ndio maana tukasema Mhe. Spika, ili tuweze kuuboresha vizuri huu mswada kwa sababu unajuwa wakati mwengine kifungu kukipitisha unaweza ukaja kukataa kwa sababu hukujibu. Lakini unakubali unapitisha kifungu ambacho una uhakika nacho.

Ndio maana tukakuomba Mhe. Spika, utumie busara zako ingawa ulisema jioni tusije labda kutoka na *schedule* yetu. Lakini kwa kuliboresha hili suala hata tukipata muda mpaka hapo jioni tukaja kuchangia vizuri itakuwa vizuri zaidi Mhe. Spika, kuliko kupitisha tu vifungu hapa.

Kamati sawa watakuwa wao tayari wameona lakini sisi wengine kwa bahati hatukupa kuchungulia tukajua tunapitisha kitu gani. Vyenginevyo naomba utumie busara zako tu Mhe. Spika. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, mimi nadhani suala la msingi ambalo linazungumzwa kwamba mswada kwa mujibu wa kanuni zetu umekuja umechangiwa ikatoka hoja kwamba urudi kwenye kamati ambazo kanuni zetu za 86-87 zinakubali utaratibu huo na sasa tumeletewa marekebisho chini ya kanuni ya 84.

Kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni hii mimi nadhani kwanza hakuna haja ya Mhe. Waziri kuwasilisha haya marekebisho kwa sababu kanuni inasema vizuri kwamba baada ya marekebisho kutengenezwa yatagaiwa tu na katibu kwa kila Mjumbe. Kila mjumbe ameshapata haya marekebisho.

Sasa ni fikira iliyotolewa kwamba kwa sababu ya marekebisho yenyewe yalivyo tunahitaji muda kutapitia tukayaoanisha na huu mswada wenyewe. Mimi nadhani mambo mawili au rai yangu ni mambo mawili tu.

Kwanza mimi nadhani ni vizuri na itatusaidia kama Wajumbe watapata muda kama ni muda huu mpaka jioni au muda huu mpaka kesho asubuhi. Hiyo ni muongozo wako utakavyoutoa.

La pili kwamba Wajumbe waliokwisha kuchangia kanuni zetu ziko wazi kwamba mswada ukichapishwa ama mara ya pili ama mswada ukiwa umetolewa marekebisho kama yalivyotolewa haya chini ya kanuni ya 84 ni yule utaona mwenyewe kwamba achangie hajachangia ndio atakuwa na fursa ya kuchangia.

Lakini aliechangia hata kama alichangia kabla ya marekebisho basi hiyo fursa ni kwamba yeye tayari ameshachangia. Hayo marekebisho atayaona yalifaa atakuwa na fursa katika kamati ya kupitisha sheria pengine kutoa maelezo au kutoa hoja yake ambayo ataiyona katika Kamati ya kupitisha sheria.

Kwa hivyo, fikira yangu mimi kwa vile imeshatimizwa kanuni yetu ya 84 kwamba orodha ya marekebisho imeshachapishwa imeshagaiwa Wajumbe wameshaona.

Sasa kama kuna haja ya kuakhirisha wakapata muda watu wakaipitia ili kama itaruhusiwa kuja kuchangia zaidi wachangie zaidi.

Lakini si dhani kwamba kuna hoja ya kuwasilishwa marekebisho haya rasmi na Mhe. Waziri na ninadhani wale waliokwisha kuchangia basi wameshapata fursa kwa mujibu wa kanuni zetu kuchangia.

Mhe. Spika: Nafikiri tukubalie kwamba tuwape muda Waheshimiwa Wajumbe mkapitie marekebisho haya jioni tuendelee na mjadala kwa wale ambao hajachangia.

Sasa na kwa sababu hizo mimi nadhani moja kwa moja tukubaliane na hoja hizi tulizozitoa na hii maana yake mnanambia kikoa hichi sasa nikiakhirishe hadi saa 11:00 jioni ambapo wale ambao watakuwa hawajachangia na nimeshamuona Mhe. Hamza Hassan Juma ni mmoja wapo atafika mapema na Mhe. Ismail Jussa Ladhu pale anaonesha na kweli hapa hayupo katika orodha ya waliochangia basi hao watakuja kuchangia hapo jioni saa 11:00.

(Saa 6:33 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tulikubaliana kufungua mjadala kidogo ili kufikia kuweza kufikia pahala tukaweza kufanya majumuisho jioni hii.
Basi naomba nimkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadae Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subuhana Wataalla kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na alaasiri hii kuendelea na mjadala wa Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuweka Sheria ya Biashara ya Zanzibar Na. 4 1989 na kuweka vifungu vya kuimarisha biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Pili, Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu lakini pia kwa busara zako asubuhi kutukubalia ombi letu kwamba kutokana na kugaiwa jadweli la marekebisho kipindi kile kile ambacho tulipaswa twende katika vifungu, tukakuomba kwamba tupate muda kidogo tupitie ili tujiridhishe kwamba kile tunachokipitisha sote dhamira yetu ipo safi juu yake.

Mhe. Spika, namna unavyokiendesha chombo hiki peke yake kinaacha sifa kubwa kwako na jinsi ambavyo umekuwa siku zote mnyumbufu (*flexible*) katika kuhakikisha kwamba chombo hichi kinatimiza malengo yaliyokusudiwa wakati kinaanzishwa.

Nikushukuru na nikupongeze kwa hilo Mhe. Spika.
Sasa Mhe. Spika, sitaki nichukue muda mrefu naomba niende moja kwa moja katika yale nilikusudia kuyachangia na hasa baada ya kupata nafasi ya kuupitia jadweli lile la marekebisho.

Lakini kabla sijaingia kule Mhe. Spika, kwa sababu nilikuwa sikuuchangia, yapo maeneo machache ambayo nilikuwa naomba vile vile katika mswada ule uliokuwa tumegaiwa nilitaka niyagusie na ningeomba nianze na kifungu cha 23 cha mswada. Mhe. Spika, kifungu hiki cha 23 (1) (a) ndio ninavyojikita hapa lakini kifungu cha 23 kwa ujumla wake kinazungumzia kile kilichoitwa wajibu wa muuzaji.

Sasa kifungu kinasema cha 23 (1)

> "Kila muuzaji au anaekusudia kuuza bidhaa au kutoa huduma kwa mtu yeyote anaetoa huduma kwa wateja kwa niaba ya muuzaji au anaekusudia kuuza atapaswa kuzingatia yafuatayo:
>
> > a) Awe na taaluma ya kutosha juu ya bidhaa au huduma inayotolewa na kuzingatia mahitaji yaliyowekwa katika uuzaji wa biashara husika;"

Hapa Mhe. Spika, nilikuwa naomba nije nisaidiwe tu na wizara watakapokuja kufanya majumuisho kwamba tunapozungumzia taaluma ya kutosha juu ya bidhaa au huduma inayotolewa tunakusudia kitu gani? Kwa sababu taaluma ni kitu mara nyingi kinakwenda kiwango fulani cha elimu. Ndio maana kidogo hapa palipotumika na neno taaluma limenitatiza nikataka kuelewa kwamba tunakusudia nini?

Mhe. Spika, inanipa shida kwa sababu mswada huu ni muhimu na unajumuisha maeneo mengi sana au kwa ujumla wake shughuli za biashara. Sasa wafanyabishara wetu wanaouza bidhaa kwa mfano tuchukue zile za huduma za kila siku ya mahitaji ya binadamu, tumezoea kuita maduka yanayotoa resheni, kwa maana ya vyakula.

Sasa tunaposema kwamba muuzaji awe na taaluma ya kutosha juu ya bidhaa, tunamtegemea muuzaji huyu awe anajua kila bidhaa aliyeiuza? Na tukichukulia kwa mfano maduka ya Darajani pale Mhe. Spika, kila kitu pale kinauzwa kwa mchanganyiko wake, sidhani kwamba kwa muuzaji au yule ambaye kamueka yeye kuuza kwa niaba yake kwamba atakuwa na taaluma juu ya kila bidhaa iliyokuwepo pale.

Sasa ninasema tusije tukaweka masharti ambayo baadae utekelezaji wake ukawa mgumu. Kwa hivyo, nilikuwa hili naomba nipatiwe maelezo juu ya nini hasa wizara imekusudia juu ya kifungu hiki cha 23 (1) (a).

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, naomba sasa nije katika kifungu cha 25 (3) ambacho hichi kimeguswa na jadweli hili la marekebisho. Haidhuru jadweli limerekebishwa kuangalia kwangu neno moja tu. Hichi kinasema Mhe. Spika, naomba nikisome kifungu cha 25 (3).

> "Kifungu cha 25 (3) Pamoja na vifungu vya sheria hii Manispaa na Halmashauri za Wilaya zinaweza kutoa taratibu nyengine za masharti kwa biashara mtaani au kufanya biashara sokoni na ikitokea mgongano wa kisheria katika vifungu vya sheria hii kati ya vifungu vya sheria hii na kanuni za mamlaka hizi sheria hii ndio itakayokuwa na nguvu"

Sasa Mhe. Spika, kamati katika jadweli lao la marekebisho wamefuta au wamependekeza kufuta neno 'kutoa taratibu nyengine', wamependekeza likae neno 'kuweka taratibu nyengine'

Lakini maudhui hayatofautiani sana. Sasa mimi sina tatizo la lugha. Tatizo langu lipo katika maudhui ya kifungu hiki. Naomba vile vile atakapokuja kufanya majumuisho nisaidiwe Mhe. Spika, ili niridhike ili nikipitishe kifungu hiki.
Wasi wasi wangu upo wapi Mhe. Spika, wasi wasi wangu upo kwamba sheria inasemwa ndio itakayoweka masharti ya uendeshaji wa biashara katika nchi yetu.

Lakini kwa kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 25 kinatoa fursa kwa Manispaa na Halmashauri za Wilaya kuweka taratibu nyengine za masharti kwa biashara, lakini imetajwa biashara ya mtaani au biashara ya sokoni.

Sasa Mhe. Spika, hapa leo asubuhi kulikuwa na swali linalohusu uendeshwaji wa biashara hasa katika eneo la Jua Kali pale Darajani. Lakini hoja yangu haihusu pale inaweza ikawa ni popote kwamba serikali kuu inaamua kama ilivyotoa tangazo kali leo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ,

kwamba ikifika tarehe mosi hataki msalie Mtume, sijui sisi tumefundishwa kumsalia Mtume kama yeye anakataa kumsalia Mtume? ninadhani sijui hata wananchi wake wa Jimbo la Tumbatu watamuelewa lakini nilikuwa nasema kwamba linakuja tatizo la wafanyabiashara wanalalamika kwa sababu gani, kwamba wanasema serikali kuu inatoa maagizo mamoja lakini mamlaka nyengine ndizo hizi tunazozipa mamlaka hapa; Manispaa na Halmashauri za Wilaya zinafanya vyengine.

Kwa mfano, pale tunaambiwa Mhe. Spika, haparuhusiwi kufanya biashara lakini watu wa Manispaa wanakwenda kutoza kodi pale mbali mbali na tozo na ada nyengine. Sasa ninajiuliza vipi mkono mmoja wa serikali unasema pale hapafai kufanya biashara lakini mkono mwengine wa serikali katika serikali za mitaa unakusanya mapato na tozo kutoka kwa wafanyabiashara wale wale ambao wanaoambiwa wanafanya biashara si kihalali.

Sasa naogopa kwamba tunapoweka vitu kama hivi, ndio yale tunajaribu kutaka kuonesha kila kitu tunakizingatia lakini matokeo yake tunaleta mgongano. Na sheria inasema ikipitishwa kwamba pakitokezea mgongano sheria hii ndio itakayosimama. Panaweza pakajitokeza matatizo makubwa sana lakini fahali wawili wakipigana Mhe. Spika, zinazoumia ni nyasi.

Sasa inawezekana katika kugombania mamlaka baina ya sheria kuu hii na mwenye mamlaka yake ambayo itakuwa ni wizara na zile sheria ndogo ndogo ambazo zilizoruhusiwa Manispaa na Halmashauri yako kuzifanya zikija kugongana anayeumia ni huyu mfanyabiashara ambaye anafanya biashara katika maeneo haya na hasa maeneo yaliyotajwa kwamba ni maeneo ya mitaani na masokoni. Mhe. Spika, nilikuwa hili Mhe. Waziri akija atutosheleze tuone kwamba hatupitishi jambo ambalo baadae linawaletea usumbufu watu, wakatozwa fedha ni kama wale wanaoambiwa wanavunjiwa nyumba wakati mamlaka nyengine zote zimeshatoa vibali vya kila aina kujenga nyumba katika maeneo hayo baadae wakaambiwa wamekiuka taratibu. Mhe. Spika, naomba hilo nisaidiwe.

Halafu Mhe. Spika, kifungu cha 33. Hichi kinahusu utoaji wa kibali cha uingizaji na usafirishaji. Hapa sina tatizo la kifungu hasa, nikitaka nikitumie kutoa indhari tu kwa wasimamizi wa sheria na serikali kwa jumla.
Mhe. Spika, kifungu kinasema 33 (1):

> "Bila ya kuathiri masharti ya sheria hii Waziri kwa kupata maombi ya utoaji wa kibali cha kusafirisha au kuingiza bidhaa au huduma nyengine yoyote kitatolewa kwa majibu wa masharti yafuatayo:

a) “Kimetolewa kwa kusafirisha au kuingiza bidhaa kwa muda maaluma na kikawekewa masharti ikiwa yapo; au
b) Kukataa kutoa kibali cha kusafirisha au kuingiza bidhaa"

Na kifungu cha 33 (2) Mhe. Spika, kinasema:

"Kibali cha kuingiza au kusafirisha bidhaa kitatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa ndani ya Kanuni ya Sheria hii"

Sasa Mhe. Spika, hapa nilitaka kusema tu kwamba tukitizama sasa hivi hali halisi na mimi sidhani ni kwa sababu ya upungufu wa sheria. Kwa hivyo, nina hakika haya hata katika Kanuni yapo haya, kwa sababu tumezoea sisi wengine tangu tukiwa wadogo wachilia mbali kutoa nje ya nchi hata kutoa sehemu tu ya nchi kwenda sehemu nyengine kulikuwa na utaratibu wazee wakiita kukata cheti, ilikuwa ni lazima upate kutoa bidhaa fulani kwenda sehemu nyengine seuze kutoa nje ya nchi. Lakini tatizo linakuja katika miaka ya karibuni katika *enforce* kutilia mkazo kutekeleza masharti yale.

Sasa Mhe. Spika, tukitazama haya katika nchi nyengine tunasafiri bahati nzuri tunaona kwamba unapokwenda katika nchi kwa mfano mazao ya kilimo katika kujaribu kuepusha kuingiza mazao yanayowea kuleta maambukizo ya maradhi kwa mimea, wanakuwa wakali kweli kweli katika kufuata taratibu zile na kama utagundulikana nayo hupiti nayo, tumeona hayo na kama huna kibali basi utapata matatito kweli kweli.

Nchi kama Marekani Mhe. Spika, ile shahada ya kuingizia katika nchi unayojaza katika Uhamiaji ambayo siku hizi unapewa ndani ya ndege katika nchi nyingi, ukisoma wanatoa shahada mbili wao; kuna shahada moja kazi yake ni kuelezea vitu ulivyochukua hasa katika mambo ya mazao tu ili kulinda kwamba afya za wananchi wao lakini pia kulinda kuja kuambukizwa maradhi ya mimea nchi zao au wanyama.

Sasa hapa pameekwa utaratibu mzuri katika kutunza biashara na vibali vyake. Lakini nilikuwa ninajiuliza ninasema wizara vipi imejipanga kuhakikisha kwamba taratibu hizi zinatekelezwa ili na nchi yetu isiwe pahala holela.
Mhe. Spika, hivi sasa hali ya bandari hasa na viwanja vya ndege tunavijua vilivyo na jinsi usimamizi wa masharti haya unapokuwa mgumu. Kwa hivyo, nilikuwa

Mhe. Spika, nikitumie kifungu cha 33 kutoa hiyo indhari.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa naomba niende kwenye lile jadweli la marekebisho katika maeneo yanayohusu makosa na adhabu ambayo ndio yaliyosababisha hasa huu mswada juzi Wajumbe wakatoa hoja kwamba uangaliwe tena.

Mhe. Spika, nilichokiona na kwa hili kwa jumla sina tatizo nalo ni kwamba marekebisho ya kamati yamefanya kwamba kila palipo na kosa pametajwa tu, kwamba mtu akifanya kitendo fulani atakuwa ametenda kosa, ile adhabu imeondolewa ili kwenda pamoja na lile pendekezo la kamati kwamba adhabu zote ziwekwe kwenye jadweli ya sheria.

Sasa Mhe. Spika, nimelipitia kwa jumla sina matatizo sana na jadweli ambalo limeekwa limetajwa mtaji wa biashara, malipo ya faini na kifungu ambacho kinaambatana nacho ambacho bila shaka ndio itakuwa muongozo kwa utaratibu ule. Lakini Mhe. Spika, kuna maeneo mawili kidogo yamenipa shida.

Moja Mhe. Spika, ni kifungu cha 50 (3) kama kilivyorekebishwa katika jadweli hili la marekebisho. Mhe. Spika, kifungu cha 50 (3) kinasema kimeongezwa kilikuwa hakipo. Kuongeza kifungu hiki kinachompa mamlaka Waziri kufanya marekebisho ya jadweli itakapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, naomba nisome mapendekezo ya kamati na hicho kifungu kipya cha 50 (3), kinasema,

> "Waziri anaweza kufanya marekebisho ya adhabu zilizoainishwa katika jadweli nambari 4 la sheria hii kila itakapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo"

Mhe. Spika, mimi kidogo hapa nimepata matatizo. Mwenye mamlaka hasa ya kutunga sheria ni chombo hiki tunachokiongoza. Bila shaka sheria mbali mbali zimekuwa zikitoa fursa baada ya kuidhinishwa na chombo hichi kuipa mamlaka Wizara kupitia Waziri kutunga Kanuni. Lakini katika jambo kubwa hili Mhe. Spika, naona haya ni madaraka makubwa sana kumpa Waziri kurekebisha jadweli ambalo linaweka adhabu ingelikuwa ni faini tu sina matatizo, lakini jadweli hili linajumuisha faini na kifungo na marekebisho yaliyoletwa hayaoneshi kwamba labda Waziri ana mamlaka ya kurekebisha adhabu katika faini, imeweka kwa ujumla wake.

Sasa naogopa kuja kufika pahala kwa sababu moja katika suala la kuzingatia ni kutunga sheria ni uwiano au proportion ya adhabu na kosa. Sasa chombo hichi kimelalamika sana kuhusu adhabu na makosa yaliyokuwemo katika mswada ulioletwa mpaka ikapelekea tuombe mswada huu urejeshwe katika kamati ili

tujiridhishe uletwe tena. Sasa tunapofika pahali leo mamlaka yale ambayo sisi tuliona kwamba ni hatari kupitisha bila ya kujiridhisha, leo tunayahamisha tunasema tunayaweka humu lakini halafu tunampa mamlaka mtu mmoja kuweza kurekeisha. Hili kidogo Mhe. Spika, ninanitisha.

Sasa mimi pendekezo langu tunaweza tukaliacha lakini katika utungaji wa Kanuni kuna masharti mbali mbali huwa yanazingatiwa, yanaweza yakawa ni masuala ya jumla sana ikasemwa kwamba Waziri atatunga Kanuni tu hasa kama ni masuala ya jumla jumla ya utawala na mambo mengine. Lakini kuna mambo mengine yanapotaka kutungiwa Kanuni ikiwa yanagusa msingi muhimu sana wa sheria basi kunakuwa na taratibu ama anaambiwa anayeweza kutunga Kanuni hizo baada ya kupata idhini ya Baraza kama chombo cha kutunga sheria au la pili angalau kwa kupata idhini ya kuthibitishwa na Kamati ya sekta inayohusika ya Baraza, na taratibu hizi Mhe. Spika, zinatumika katika nchi nyengine vile vile.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninataka kupendekeza kwamba haya madaraka makubwa sana ya kifungu cha 50 (3) kilichopendekezwa kuongezwa kumuachia Waziri peke yake. Mimi nilikuwa ninapendekeza kama lazima basi angalau kiseme kwamba Waziri ataweza kufanya marekebisho ya adhabu hizi lakini baada yaani *subject to*, baada ya kupata ridhaa au idhini ya Kamati inayohusika kwamba imeridhika. Nilikuwa ninadhani hilo ni muhimu sana ili tusitoe madaraka haya makubwa kwa mtu mmoja.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni kifungu cha 51 (4). Hichi Mhe. Spika, kinazungumzia naomba nikisome adhabu ya papo kwa papo. Hichi kifungu kinasema hivi, kifungu cha 51 (4) kama kilivyorekebishwa:

> "Taarifa chini ya kijifungu cha 1 cha kifungu hichi zitainisha makosa yanayodaiwa na kutoa maelezo ya msingi dhidi ya makosa hayo na pia itaeleza muda ambao matokeo hayo hayatochukuliwa hatua na kueleza kiwango cha adhabu ya papo kwa papo na kuainisha anuani ya ofisi ambapo malipo yanatakiwa kufanywa"

Hichi ndicho kilivyorekebishwa na kamati Mhe. Spika, lakini kwa jumla mimi nimepata matatizo na hii *concept* au dhana ya adhabu ya papo kwa papo hasa baada ya kuangalia uzoefu katika nchi yetu.
Mhe. Spika, ili nifahamike naomba nikisome hichi cha 50 (1) ambacho ndio kifungu mama au ndio kijifungu mama cha kifungu hichi. Kinasema:

"Endapo Mkurugenzi anazo sababu za kuamini kwamba mtu yeyote ametenda au anatenda kosa ambalo sheria imelionesha kuwa ni kosa Mkurugenzi anaweza kumpa taarifa ya maandishi yenye kuonesha kwamba anatiwa hatiani kwa kosa lake hilo kwa kulipa faini kwa adhabu ya papo hapo na mtu huyo hatokuwa tena na mwenye hatia kwa kosa hilo ikiwa adhabu ya papo hapo imetekelezwa kwa mujibu wa kifungu cha sheria hii kabla ya kumalizika kwa siku 14 baada ya siku iliyotolewa taarifa hiyo au kabla siku ambayo shauri halijaanza kusikilizwa Mahakamani kwa tukio lililotokezea isipokuwa mtu huyo aliyedhibitiwa katika kifungu hichi sio Mzanzibari sio Mkaazi wa Zanzibar adhabu ya papo hapo itatakiwa ilipwe mara tu baada ya tukio".

Sasa Mhe. Spika, mimi kidogo muoga wa madaraka kama haya kumpa mtu mmoja. Mhe. Spika, naogopa sana kwa kifungu hichi kuja kushindwa kutilia nguvu ukiukwaji wa sheria kwa kivuli cha adhabu ya papo kwa papo ambayo haitopelekea watu kupata *incentive* au motisha ya kutekeleza sheria.
Mhe. Spika, nini ninachokusudia, ninahofia rushwa sina haja ya kuficha.

Mara nyingi tumeona sheria kama hizi au Kanuni kama hizi ambapo zimempa mamlaka mtu mmoja kufanya maamuzi kama haya Mhe. Spika, binadamu ni binadamu anaweza huyu akaja akawa *compromise* akapewa vishawishi vya rushwa, mtu akafanya makosa makubwa sana na pengine anaumiza binadamu, kwa sababu tukizungumza biashara kuna mambo mengi sana hapo ndani yake. Lakini akaamua kukwepa mkondo wa sheria kwa sababu ya kupewa adhabu ya papo kwa papo ambayo mlango wake umeachwa wazi mno na kifungu hichi 51.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba hichi tukiangalie tena na Mhe. Waziri akija atusaidie maelezo ya hili.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, ninasema nikipata maelezo hayo sina tatizo na ninaomba nimalizie kwa kusema kazi kubwa imekuwa nyepesi kwa sababu ya kazi ambayo imefanywa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Kwa hivyo, ninaipongeza kwa kazi kubwa iliyochukua na jitihada iliyofanya ya kuupitia tena kwa kina mswada huu baada ya kurejeshwa kwao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema nikipata maelezo ya kuridhisha katika vifungu hivyo nilivyovitaja basi sina matatizo naunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia.

Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi ninataka niungane na mwenzangu aliyekaa kutoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kuwa mnyumbulishi kama lugha alivyoitumia mwenzangu. Mnyumbulishi anaulizwa kwa lugha ya Kiswahili maana yake ni mtu ambaye anakubali ushauri, sio kang'anga'na tu anachokitaka yeye ndiye hicho hicho, haa! Pale ambapo anahisi wenzangu wamenishauri vizuri basi anatusikiliza pamoja kwamba yeye ametuzidi kwa kila hali; kwa maarifa, umri na kila kitu. Kwa hivyo, tunakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kutulea vizuri.

Mhe. Spika, na mimi kama nilivyosema mwanzo naipongeza sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kuweza kuupitia kwa kina mswada huu na kufanya marekebisho mengi. Sasa na mimi nilikuwa tu nina baadhi ya masuala mawili matatu pamoja na ushauri ili tumuachie Mhe. Waziri aendelee kukamilisha majumuisho.

Mhe. Spika, mimi ninakuja moja kwa moja katika mswada huu ukurasa wa 279 inayoosema sehemu ya pili Idara ya Biashara. Mhe. Spika, hapa kifungu cha 4 (1) kinasema:

4(1) "Inaanzishwa idara itakayokuwa na majukumu ya uendeshaji wa biashara itakayojulikana kama Idara ya usimamizi wa biashara.

(2) Kutakuwa na na mkurugenzi ambae atateuliwa na Rais.Na hapa chini zikatekelezwa sifa zake”

Mhe. Spika, mimi hapa nilikuwa ninataka nipate ufafanuzi. Katika kumbukumbu zangu ninaona kama tunayo Idara ya Biashara au hii Idara ya Biashara haipo kama ipo kwa kuwa inaundwa tena kwa sheria, sijui utaratibu wake ukoje, kwamba kama idara ipo halafu inaundwa tena.

Kwa kuwa vile vile kuna mkurugenzi ambaye ametajwa atateuliwa na Rais basi ninataka nijue kama Idara hii ya Biashara ipo ilikuwa na mkurugenzi au ilikuwa haina, na kama alikuwepo kwa kuwa sheria hii inataja kwamba kutakuwa na mkurugenzi atateuliwa na Rais, sijajua kama atateuliwa tena au vyenginevyo. Hapa tu kidogo nilikuwa ninataka maelezo.

Lakini chengine Mhe. Spika, katika ukurasa huu huu kifungu cha 4 (3) kinachosema kwamba,

"Mtu atakuwa na sifa ya kuwa mkurugenzi ikiwa" hapa chini imeeleza

a) Angalau shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu ya Uendeshaji Biashara au Uongozi wa Biashara au Uchumi au Sheria ya Utawala ya Umma.

Mimi tu hapa nilikuwa ninasisitiza Mhe. Spika, kwamba hizi sifa tunazozitaja katika sheria ninaomba sana zitekelezwe kama zilivyo kwa sababu kumekuwa na tatizo kuna baadhi ya hawa wakurugenzi ambao sheria sifa inataka awe na viwango fulani vya shahada, matokeo yake wanapewa watu ambao hawana viwango vile, matokeo yake wanatusumbua sana katika utekelezaji na usimamizi wa majukumu yao ya kila siku.

Kwa hivyo, hili tu nilikuwa ninaliomba kwa sababu hizi sifa na elimu zinazotajwa bila shaka kuna taaluma ambayo mtu anakuwa nayo akishakabidhiwa haya majukumu hawezi kuleta taabu.

Lakini jengine Mhe. Spika, nilikuwa nimejaribu kuangalia sehemu ya tatu katika ukurasa wa 281. Sehemu ya tatu yaani Baraza la Ushauri. Kifungu cha 6 kinasema,

> "Kutakuwa na Kamati ya Ushauri ya Biashara chini ya idara kwa ajili ya kutoa ushauri kwa ujumla katika kukuza na uendeshaji wa biashara Zanzibar".

Hapa kifungu cha 7 (1) kinasema:

> "Kamati ya Ushauri itakuwa na wajumbe hawa wafuatao ambao watateuliwa na Mhe. Waziri"

Hapa kuna orodha ndefu kuanzia (a) mpaka (j); kuna mwenyekiti, wizara inayohusika na kilimo, kamati wamefanya marekebisho hapa baada ya kwamba ni wizara inakuja ni mjumbe. Ninakubaliana na marekebisho hayo.

Sasa hapa hoja yangu ipo moja kwamba hawa wajumbe naona ni wengi sana ndio hapa nitakapokuja kutaka ufafanuzi. Kwa sababu ukiangalia hata sheria ya mitaji ya umma tuliyoipitisha hapa ya 2002 ilikuwa inaeleza, mfano kama kutakuwa kuna bodi basi aidha wajumbe wasizidi saba na wasiopua watano.

Sasa jee, sheria ile ya mitaji ya umma haiwezi ika-*applied* katika eneo hili kwa sababu tunaona hii kamati itakuwa na wajumbe wengi sana. Lakini vile vile katika eneo hili hili, hapa kuna kifungu cha 7 (4) kinasema:
"Mwanasheria kutoka katika wizara atateuliwa kuwa Katibu wa kamati"
Lakini huku samahani kidogo, kifungu hichi kilikuwa kinazungumza kwamba kifungu cha 7 (2):

> "Mtu atakuwa na sifa ya kuwa mwenyekiti wa kamati akiwa angalau shahada hizi ambazo zilizotajwa hapa chini”

Lakini kifungu cha 7 (3) kinasema:

"Mkurugenzi atakuwa ni mjumbe wa kudumu wa kamati na kwa kushauriana na Katibu wa Kamati ataratibu shughuli zote za kamati"

Lakini sasa huku Mhe. Spika, kwenye kamati kifungu cha 7 (3) wao walifanya masahihisho na inaonesha Mhe. Waziri aliyakubali. Lakini mimi masahihisho haya naona bado sijayakubali kwamba kamati imesema kwamba mkurugenzi atakuwa ni Katibu wa kudumu wa kamati na ataratibu shughuli zote za kazi za kamati.

Sasa mimi ninadhani yale mapendekezo ya Mhe. Waziri, yale ndio yaliyokuwa sahihi kwamba ile kamati ndio itateuwa Mwanasheria katika wizara ili awe Katibu wa Bodi, kwa sababu mkurugenzi leo kumfanya ndio Katibu wa kamati ina maana unampa majukumu mengine. Mkurugenzi katika hii kamati yeye anakuwa kama ni afisa kutoka katika wizara. Lakini sasa ikiwa mkurugenzi utamchaguwa kuwa ndiye katibu wa bodi, katibu wa kamati mimi nafikiri inakuwa sio sahihi sana.

Mhe. Spika, mimi pia nina uzoefu, niliwahi kuwa mjumbe wa bodi ya Shirika la Bandari kwa vipindi karibu viwili, basi mkurugenzi anakuwa ni *X official*, yeye anakuwa ni mtendaji katika ile taasisi na anawajibika katika ile kamati. Sasa ikiwa mkurugenzi yeye anawajibika kwa ile kamati, halafu yeye ndio anakuwa katibu wa ile kamati, mimi nafikiri sio sahihi. Kwa hivyo, mimi hapa kidogo natafautiana na mawazo ya kamati, bado nilikuwa napendekeza kwamba mkurugenzi awe ni mjumbe wa kudumu katika hiyo kamati, lakini ateuliwe mwanasheria kutoka katika wizara ambaye ndiye atakayekuwa ndio katibu wa hiyo kamati ambaye ataweza kuweka hizo kumbukumbu kama maelezo yaliyoelezwa. Kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba kifungu cha 7(4) na 7(3) visifutwe na vibakie kama vilivyo.

Eneo jengine….

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya muda sio mrefu tunategemea Mhe. Waziri baada ya Mhe. Naibu Waziri kuchangia na yeye shughuli hii ili tuikamilishe. Sasa nawaangalia Wajumbe wangu hapa, wengine wanaingia na wengine wanatoka, hali ya *quorum* bado haijawa nzuri. Kwa hivyo, niwaombe Wajumbe waliopo nje warudi ndani ili tumalize kazi. Mhe. Hamza Hassan Juma endelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nadhani labda huo mkahawa ufungwe kwa wakati wa kazi ili wajumbe waendelee kubakia humu ndani.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nilikuwa nakuja katika kifungu cha 8(1) kazi za kamati. Kamati itatowa ushauri kwa ujumla kwa wizara katika haya mambo ambayo yanafuata. Uandaaji wa sera na mambo mengine na ndio maana pale nikapendekeza kwamba mkurugenzi yeye asiwe katibu wa bodi, kwa sababu hii kamati bado ina kazi ya kuishauri wizara na wakati mkurugenzi yeye ni miongoni mwa hao watendaji wa hiyo wizara. Kwa hivyo, hapa kifungu cha 8(1)(h) yaani hapa kamati itatoa ushauri kwa ujumla kwa wizara katika mambo hayo hapo chini, kukuza viwanda, usanifu wa biashara, kuuza soko la ndani, afya ya jamii.

Lakini (h) kinasema:

> "Shughuli nyengine yoyote itapangiwa na Waziri au Katibu Mkuu wa Wizara"

Sasa Mhe. Spika, kamati kufanya shughuli nyengine yoyote ambayo imepangiwa na waziri sina tatizo. Lakini kamati kufanya shughuli nyengine yoyote iliyopangiwa na Katibu Mkuu, hapa kidogo naona sio sahihi. Kwa sababu hii kamati ameiteua Mhe. Waziri, kwa hivyo, moja kwa moja inawajibika kwa waziri. Sasa leo utakaposema kwamba itapokea maagizo aidha kwa waziri au na Katibu Mkuu. Mimi nadhani hapa inawezekana Katibu Mkuu kuiagiza kamati pengine hakushauriana na waziri ikaja kuwa na mgongano wa mawazo katika mambo ya utendaji.

Kwa hivyo, mimi nadhani kama Katibu Mkuu yeye anahisi kuna wazo anataka kuipa kamati ili ilifanyie kazi, moja kwa moja ni kumshauri Mhe. Waziri, na Mhe. Waziri yeye ndiye aiagize kamati ili iweze kufanya kazi hiyo ambayo imepangwa. Sasa nilikuwa naomba kifungu cha 8(h) hayo yalikuwa ndio mapendekezo yangu, yaani kifungu hiki kubakia kama kilivyo, nahisi itakuwa sio sahihi sana.

Mhe. Spika, vile vile kifungu cha 9(1) kinasema mkutano wa kamati:

> "Kamati itakutana katika kutekeleza wajibu wake kwa muda na sehemu itakayoamuliwa, lakini kwa namna yoyote ile watakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu”

Sasa huku mbele hakukuwa na *exemption* nyengine ambao utakuwa aidha kuainisha vikao vya dharura. Sasa na sheria ndio sheria, sheria ukishaitaja kwamba kutakuwa na kikao kimoja au mkutano mmoja katika kila baada ya miezi mitatu, endapo itatokea haja hukuweka *exemption* hapa kwamba wanaweza wakafanya

kikao cha dharura, mimi nafikiri hapa watakuja kushindwa kufanyakazi, pengine kutakuwa kuna jambo muhimu kabisa, wanataka kumshauri waziri pengine wakati wa bajeti unakaribia, lakini kikao wale walikwishakukaa ndio wazo limekuja. Sasa mimi nadhani iwekwe na *exemption* hapa kwamba kamati vile vile ikiwa kuna jambo la dharura wanaweza wakakutana wakati wowote.

Mhe. Spika, pia kifungu cha 9(2) kinasema kwamba:

> "Kutokuwepo kwa mkurugenzi au mwenyekiti makamu mwenyekiti anaweza wakati wowote kuitisha mkutano wa dharura wa kamati pale ambapo kuna ombi la maandishi kwa wajumbe walio wengi wa kamati ndani ya ofisi"

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 9(3) kinasema:

> "Mwenyekiti, au pale ambapo mwenyekiti hayupo, makamu mwenyekiti anaweza na kwa maombi ya wajumbe walio wengi kumualika kwenye mkutano mtu yeyote ambaye si mjumbe kushiriki katika jambo lililokusudiwa na kamati, lakini mtu huyo hatostahiki kupiga kura"

Sasa hayo yote nilikuwa sina haja nayo, wazo langu hapa ni kwamba katika ile *shadow* ya uundaji wa hii kamati, kulikuwa kuna mwenyekiti na wajumbe wengine kutoka katika taasisi mbali mbali, lakini hakuelezwa makamu mwenyekiti wala hakuna kifungu kinachosema kwamba wajumbe baada ya kuteuliwa na Mhe. Waziri, watamteuwa makamu mwenyekiti miongoni mwao.

Kwa hivyo, suala hili nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kwa sababu sheria imemtaja mwenyekiti tu, lakini wajumbe hawakupewa mamlaka ya kumteuwa makamo mwenyekiti, pale baada ya kuteuliwa. Lakini huku naambiwa mwenyekiti akiwa hayupo, basi pale ambapo makamu mwenyekiti yupo anaweza akaitisha kikao baada ya kupata maombi ya wajumbe waliokuwa wengi. Sasa labda upatikanaji wa mwenyekiti hapa utakuwepo katika eneo gani.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu hiki hiki cha 9(5) kinasema:

> "Katibu atakuwa na wajibu wa kuweka kumbukumbu zote za vikao vilivyofanywa na kamati"

Kwa hivyo, hapa ndio kamati ilipendekeza kwamba kuongezwa kifungu cha 9(7) ambacho kinasema:

"Mkurugenzi atawajibika na kuandaa ripoti ya mkutano wa kamati baada ya miezi mitatu kuwasilisha kwa Waziri"

Sasa mimi nadhani kama nilivyoeleza pale mwanzo, nafikiri jukumu la kuandika ripoti na kuwasilisha kwa waziri liwe kwa yule katibu wa bodi au katibu wa kamati ambaye atakayeteuliwa na wajumbe. Kwa sababu mara nyingi katibu anawajibika kwa kile chombo anachokifanyia kazi na kwa kuwa kuna mwenyekiti pale, katibu moja kwa moja anawajibika kwa mwenyekiti. Sasa pale mfano mkurugenzi atakuwa yeye ndiye anatakiwa kuandaa hiyo ripoti, mimi nafikiri bado uwajibikaji wake kwa mwenyekiti pale, kwa sababu na yeye ana majukumu mengine, kidogo italeta utata.

Maana yake kama hapa kwenye kifungu cha 10 kinasema:

"Kamati itapokea fedha kutoka katika idara inayohusika"

Sasa hapa nafikiri idara inayohusika ndio itakuwa ile ile idara ya biashara, sasa haiwezekani mkurugenzi yeye ndio anasimamia kule katika masuala ya biashara, halafu yeye akatoa tena fedha kuikabidhi hii kamati. Kwa hivyo, mimi nadhani hapa kidogo kulikuwa kuna mkanganyo nilikuwa naomba ufafanuwe.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, ni kuhusu hapa katika Sehemu ya Nne ambayo inahusu Mamlaka ya Usimamizi, katika kifungu cha 12(1):

"Idara itakuwa na mamlaka ya jumla ya usimamizi katika kutilia nguvu sheria hii"

Kifungu cha 12(2):

"Mamlaka zifuatazo kwa kusaidiana na idara bila ya kuathiri masharti ya sheria hii na sheria zilizoanzisha mamlaka hizo kuwateuwa watu maalum ndani ya mipaka ya uwezo wao kufanya kazi ya usimamizi juu ya kushikamana na sheria hii na mahitaji mengineyaliyoanzishwa katika msingi huo, mamlaka hizo ni hizi zifuatazo"

Sasa hizi mamlaka zenyewe ni hizi hizi ambazo zinatoa wajumbe watakaokuwa katika ile kamati, halafu leo mamlaka hizi hizi zitatakiwa ziteuwe wajumbe wengine kutoka katika mamlaka zile nyengine.

Mhe. Spika, mimi hofu yangu moja hapa, kusije kukawa na mgongano wa kazi, kwa sababu hawa majukumu yao yameelezwa huku chini kwamba itateuwa idadi ya kutosha maofisa wake kila idara, wasimamizi wa biashara na bidhaa za huduma. Kwa hivyo, katika majukumu yao watakuwa wanakwenda kufanya ukaguzi katika sehemu mbali mbali, wakati huku kuna hii taasisi ya madawa na vipodozi, wao wana wakaguzi wao, kuna taasisi sijui ya kumlinda mlaji wana wakaguzi wao na nyengine ya mambo ya mizani wana wakaguzi wao.

Sasa je, na hawa kwa sababu ukiangalia watu wenyewe watendaji ndio hawa hawa, sasa si itakuwa kila siku hao wenye maduka wetu watakujakuwa ndio ule usumbufu, maana yake itakujakuwa kama yale masuala ya kodi. Leo anakwenda ZRB, kesho asubuhi anakwenda TRA.

Sasa kwa kuwa kuna zile taasisi ambazo zina wakaguzi kama hizo nilizozitaja, mamlaka ya vipodozi, mamlaka ya kumlinda mlaji na wengineo. Sasa na hii kazi yao itakuwa ndio ile ile. Hapa kidogo nilikuwa nahitaji maelezo.

Jengine la kumalizia kabisa ni kifungu cha 14(1) kinasema:

> "Msimamizi anaweza kutoa amri ambazo wauzaji, wafanyabiashara na waandaaji wa biashara watapaswa kuzifuata ikiwa;
>
> (a) “Mfanyabiashara au muuzaji anajishughulisha na bidhaa au huduma ambazo hazikufikia viwango"

Mhe. Spika, kuna mfanyabiashara mmoja hapa analeta mafuta ya kula, huyu anaagiza mafuta kutoka Indonesia, kutokana na ushindani wa biashara na pengine na fitina za biashara zilianza kuandikwa bidhaa zake kwamba hazina kiwango. Yeye mwenyewe kwa kuwa matoleo yale yalipotoka tayari alikuwa ana *stock* kubwa ghalani kwake, matokeo yake ile taasisi ambayo inasimamia viwango ikamtaka aje akaguliwe na alipokuja kukaguliwa ikabidi sasa katika sheria zao wanasema kwamba lazima yale mafuta yakakaguliwe kule sehemu ambapo yalipotoka, gharama zile inabidi azibebe yule mwenye mali na alifanya kazi hiyo na alitakiwa awasafirishe watu wawili hao TBS wenye hivyo viwango na yeye akakubali akatoa gharama za kuwasafirisha wajumbe wawili.

Lakini matokeo yake alikwenda mjumbe mmoja, yeye katoa gharama za kuwasafirisha watu wawili kwenda huko sijui Malasia yalikotengenezwa hayo mafuta, matokeo yake amekwenda mtu mmoja. Baada ya kufika kule akafanyakazi

ya ziada ambayo sio aliyotumwa, yeye alikwenda akakusanya zawadi nyingi ambazo hata katika zile kilo anazotakiwa zikawa zimezidi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hata ile *sample* aliyotakiwa aende akakaguwe pia hakuileta. Yeye kaenda kule kanunua zawadi karudi, *sample* hakuileta, wakati huku mfanyabiashara tayari amekwishakula gharama za kuwasafirisha watu wale. Mhe. Spika, hapa mimi nilikuwa natoa hayo maelezo, naamini Mhe. Waziri pengine huyo muhusika aliwahi kuonana naye, kwa sababu ule unakuwa ni usumbufu kwa wale wafanyabiashara. Kwa sababu kama kitu mnawasi wasi nacho basi nendeni mkakikaguwe mchukuwe *sample* mlete. Lakini watu wawili wametumwa anakwenda mtu mmoja na hiyo *sample* vile vile hakuja nayo. Sasa huu unakuwa ni usumbufu.

Mhe. Sika, lakini nakusudia kusema kwa mfano huo, kwamba hawa watu ambao tunawatungia hii sheria basi na wao wasije wakatumiwa na wafanyabiashara wengine, ili wazuwia na kuwadhibiti wafanyabiashara wengine wasiweze kufanya shughuli zao.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema nilikuwa sina mchango mkubwa sana na huu mswada kwa kweli nilipata kuupitia baada ya marekebisho nusu tu, lakini na wenzangu wakawa wameona maeneo mengine, nakubaliana na mapendekezo hayo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na maelezo ya ufafanuzi wa Mhe. Waziri nitaunga mkono mswada huu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi jioni hii ya leo niweze kuzungumza machache katika mswada wetu huu wa biashara.

Mhe. Spika, nataka nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana wajumbe wote 13 waliochangia mswada wetu. Lakini niishukuru zaidi kamati ambayo tumefanya nayo kazi kwa muda wote kama alivyoeleza Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Spika, mswada huu unaonekana kwamba ni mgumu, lakini haukuwa mgumu wa hivyo, isipokuwa tatizo lilijitokeza zaidi katika tafsiri. Kama alivyoeleza mwenyekiti ni kwamba wanasheria ambao tulikuwa tufanyekazi nao, kumbe wengi wao ni waajiriwa wapya kwa hivyo ni wageni katika shughuli hizi. Kwa hivyo, masuala ya tafsiri ilikuwa mara nyingi mpaka tushauriane. Hilo ndio lililopelekea pamoja na kuchelewa kuchapishwa mswada huu ambapo hatimaye ilibidi shughuli

za kukata huu mswada kuuweka katika makabrasha mashine ikagoma na ikabidi iende ikakatiwe Dar es Salaam. Kwa hivyo, yote hayo yalikuwa ni kati ya sababu zilizosababisha mswada huu hapa na pale uweze kuchelewa hadi leo hii.

Mhe. Spika, nashukuru sana michango yote iliyotolewa, Mhe. Waziri atakuja kuisema mmoja mmoja kadiri ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wamechangia. Lakini mimi nasema kwamba kilichopelekea zaidi Mhe. Spika, juzi mswada huu turudishiwe ni suala la ku-*categories* zile adhabu katika lile jadweli. Suala hili tulikaa na kamati na tukalifanyia kazi kwa pamoja, kwa sababu iweze kuingia kwenye Hansard, basi tulishauriana na Mhe. Waziri tuweze kuisoma hapa ili iwe kwamba imetoka ndani ya Baraza lako tukufu.

Vile vile, Mhe. Spika, tumekubaliana na tukaweka katika mafungu 6 kufuatana na uwezo wa mfanyabiashara au mtaji au aina ya biashara anayoifanya yule mfanyabiashara. Tumesema kwamba kutakuwa na adhabu za aina sita. Malipo ya faini shilingi 20,000 mpaka 50,000 kwa wafanyabiashara ambao mtaji wao utakuwa kati ya shilingi 50,000 mpaka shilingi 500,000. Lakini faini itaongezeka kutoka shilingi 50,000 mpaka shilingi 200,000 kwa wale wafanyabiashara ambao mtaji wao utakuwa ni shilingi 500,000 mpaka shilingi 2,000,000.

Pia, tulikubaliana kuwe na *category* ya tatu ambapo hapa mfanyabiashara akishaonekana kwamba ameingia hatiani basi faini yake itakuwa ni shilingi 200,000 kama biashara yake ni ya mtaji wa shilingi 2,000,000 mpaka shilingi 10,000,000.

Mhe. Spika, kama biashara ya shilingi 10,000,000 mpaka shilingi 50,000,000 kama mfanyabiashara ataingia katika hatia basi atalipa faini ya shilingi 500,000 mpaka shilingi milioni 1,000,000 kufuatana na kosa lenyewe na kwa mfanyabiashara mwenye biashara ya kuanzia shilingi 100,000,000 na kuendelea basi huyu kufuatana na kosa atalipa faini kuanzia shilingi 5,000,000 lakini isije ikazidi shilingi milioni 10,000,000.

Nilisema niyasome hayo Mhe. Spika, ili kuweka Hansard yetu sawa sawa na niendelee kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao na maelekezo yao. Mimi niseme kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia 100, nawaomba na Waheshimiwa Wajumbe tuungane pamoja katika kupitisha vifungu hivi ili hatimaye mswada huu baada ya kuwekwa saini na Mhe. Rais uweze kuwa sheria.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia katika jioni hii kuwa wazima wa afya na tukaweza kujadili waraka huu muhimu wa sheria yetu ya biashara Zanzibar, ambayo tumebadilisha ile sheria nambari 4 ya mwaka 1989 na kuanzisha sheria mpya ya mwaka 2013 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, vile vile, tunakushukuru wewe kwa kutupatia fursa hii adhimu tangu asubuhi ya leo kutupa nafasi nzuri Waheshimiwa Wawakilishi kuweza kutoa waraka huu ili marekebisho haya yaweza kuwa bora zaidi katika waraka huu.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu vile vile niwataje wajumbe ambao wamo katika Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo. Tunamshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii, Makamu Mwenyekiti wake pamoja na wajumbe wote kwa kutupatia mawazo yao mazuri kabisa katika kuboresha waraka huu. Nawaambia ahsanteni sana na mmetusaidia sana.

Mhe. Spika, kamwe ile kazi ya kuahirisha haikuwa kazi ya kubabaisha, ilikuwa ni kazi nzuri na ambayo imeleta sheria hii sasa hivi naamini itakuwa sheria nzuri na itakayokubalika. Zaidi ya hayo Mhe. Spika, naomba uniruhusu niwashukuru kwa dhati wale wote waliochangia katika waraka huu au mswada huu, nikianza na:

1. Mhe. Salmini Awadh Salmin
2. Mhe. Hija Hassan Hija
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Salma Mohamed Ali
5. Mhe. Ussi Jecha Simai
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Mohamed Haji Khalid
8. Mhe. Asha Bakar Makame
9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said
11. Mhe. Farida Amour Mohamed
12 Mhe. Marina Joel Thomas
13 Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Mhe. Spika, michango yao na mawazo yao tunayathamini sana na tumeyaingiza katika namna yanayostahiki katika sheria hii na ninaamini kwamba watakubalianana na sisi kwamba michango yao tumeiingiza na itatusaidia sana katika kuanzisha sheria hii.

Vile vile, Mhe.Spika, tunasema kwamba mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali wa Baraza lako, pamoja na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mahasusi katika vifungu vyenyewe hasa tumeviweka katika jadweli ambalo tumelileta la marekebisho ambalo kila mjumbe amelipata hivi leo mchana kifungu hadi kifungu.

Mhe. Spika, kuhusu hoja za jumla zilizotokeza, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja hizo kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nafikiri tutakubali kwamba ni kweli kwamba mswada huu umewafikia wajumbe kwa muda mfupi kinyume na utaratibu wa kawaida kama kanuni za Baraza zinavyoeleza, tunaomba radhi sana kwa hili na kwa heshima yako tunaomba mtusamehe.

Jengine Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba katika sheria hii kuna haja kubwa ya kuwa na kanuni. Kwa hivyo, tunaahidi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba kanuni za sheria hii zitatungwa pindipo Rais akitia saini tu basi na kanuni zitakuwa tayari. Kwa hivyo, tunaahidi kuwa kanuni na sheria zitakwenda sambamba, kwa sababu wajumbe wengi wamesisitiza kwamba kanuni ni muhimu sana zipatikane mapema. Kwa hivyo, tunaahidi mbele ya Baraza hili kwamba kanuni zitafuatana na sheria hii pale itakapotiwa saini basi na kanuni zitakuwa tayari.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu maombi kuwasilishwa kwa waziri yanasababisha ucheleweshaji. Nasema kwamba anapotajwa waziri katika sheria hii na sheria nyengine huwa inazungumzia wizara kama taasisi katika kutekeleza majukumu yake, hivyo waziri anakuwa na watendaji wake mbali mbali wakiwemo makatibu wakuu, wakurugenzi na maombi huenda katika sekta mbali mbali kulingana na utaratibu ambao waziri ataweka baada ya kupitishwa kwa sheria hii. Kwa hivyo, kumtaja waziri katika vifungu mbali mbali ni sahihi hasa kwa maombi ya vibali kwa bidhaa ambazo zimedhibitiwa na mambo ambayo ni nyeti ya bidhaa muhimu. Kwa hivyo, kwa bandari nyingi husababisha ununuzi wa bidhaa zisizokuwa na viwango.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba nchi yetu ina bandari nyingi zisizorasmi ambazo zinaingiza bidhaa zisizokuwa na viwango pamoja na bidhaa zisizoruhusiwa kama tindikali na nyenginezo. Hii ni changamoto kubwa hasa kwa nchi nyingi za visiwa kuwa na udhibiti wake inakuwa ni vigumu sana. Hivyo, kuna haja kubwa ya kushirikiana baina ya serikali na vyombo vyake pamoja na wananchi katika kudhibiti uingizwaji wa bidhaa hizo hasa katika bandari zisizoruhusiwa kwa kutoa taarifa na ufuatiliaji.

Kuwepo kwa bidhaa chakavu. Mhe. Spika, ni kweli katika nchi yetu kuna ongezeko kubwa la bidhaa chakavu ambazo zinauzwa katika soko. Katika kusimamia suala hili taasisi ya viwango Zanzibar kwa kushirikiana na idara ya mazingira zitahakikisha zinaweka viwango vya bidhaa hizo kwa ajili ya kudhibiti uingizwaji wa bidhaa chakavu ili zisilete athari kwa watumiaji na mazingira. Natumaini kuwa hali hiyo itasaidia kuona kwamba bidhaa zote zinazoingiwa zinafikia viwango vinavyokubalika. Mhe. Spika, tutadhibiti hali hii, tutataka bidhaa zilizotumika na sio kachara. Bidhaa kachara Zanzibar hazitoingia kabisa kabisa.

Kupiga marufuku uingizwaji wa nguo za ndani za mitumba. Suala hili vile vile lilizungumzwa na wajumbe wengi walipendekeza haja ya kupiga marufuku nguzo za ndani za mitumba, hasa zinazotumiwa na akinamama. Tunakubalia na hoja hiyo moja kwa moja, mswada wa sheria hii umeziweka bidhaa hizo katika kundi la bidhaa zilizopigwa marufuku katika jadweli nambari 1.

Mhe. Spika, bila kuficha hizi nguo za ndani za wanawake na wanaume zote tumezitia katika kundi la kupiga marufuku. Kuanzia Vascodagama, chupi za kike na kiume, soksi za aina zote, *body title*, fulani za ndani zote, kwa ufupi nguo zote za ndani tutazipiga marufuku na tutajaribu kuzitia katika sheria hii kama vile wajumbe walivyoomba.

Mhe. Spika, kuwepo kwa kamati nyingi katika utendaji. Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake taasisi yoyote ile ni muhimu kuunda kamati katika kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa malengo yaliyowekwa. Utaratibu huu wa kuunda kamati hutumika hata katika mabunge na Mabaraza ya Wawakilishi ili kufuatilia na kusimamia vyema utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, uundwaji wa kamati ulielezwa katika sheria hii na sheria nyengine uko sahihi, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote wakubaliane na sisi kwamba kamati hizi ni muhimu.

Sheria ya kumtaja mkurugenzi peke yake bila ya wafanyakazi. Mhe. Spika, mkurugenzi ni kama taasisi hawezi kufanyakazi peke yake, anasimamia kutekeleza majukumu yake ya idara hiyo. Kwa hivyo, kunakuwa na muundo wa idara pamoja na wafanyakazi mbali mbali, mambo ambayo sio lazima kuyaeleza katika sheria kama hii.

Mhe. Spika, kuhusu mashirikiano na taasisi nyengine katika udhibiti wa bidhaa. Mhe. Spika, ni kweli kuna haja kubwa ya kuweka ushirikiano katika kusimamia uuzaji wa bidhaa, usambazaji wa bidhaa na mambo mengine yanayohusu biashara

ambayo yametajwa katika sheria hii. Kwa hivyo, idara ya biashara katika kusimamia mambo haya itashirikiana na taasisi nyengine mbali mbali za serikali na binafsi kama inavyoelezwa katika kifungu cha 12 cha mswada wa sheria hii.

Mhe. Spika, kuhusu kutengwa sehemu maalum kwa ajili ya wanyama na mimea ndani ya masoko. Suala hili sisi tunakubaliana nalo moja kwa moja kuwa ni muhimu na tumelifanyia kazi kwenye sheria hii.

Mhe. Spika, kuhusu utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi. Mhe. Spika, hili limeelezwa na hata sasa hivi mchangiaji Mhe. Ismail Jussa Ladhu, amelieleza. Taaluma hii Mhe. Spika, sio itolewe kwa wauzaji tu, hata wanunuzi ni lazima wawe na taaluma ya kununua na kuchagua bila ya kudhulumiwa au kudhulumu.Ni kweli kwamba suala la kuwapatia mazingira mazuri wafanyabiashara linakwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara na wanunuzi. Kwa hivyo, wizara itasimamia suala hili katika utekelezaji wa mswada wa sheria hii.

Aidha mswada wa sheria hii kwenye kifungu cha 5(i)(f) umeweka msingi wa kuzitaka mamlaka husika kutoa taaluma na uelewa juu ya masuala ya biashara pamoja na taaluma kuhusu uendeshaji wa biashara na utafutaji wa masoko.

Adhabu ziweke kiwango cha mtaji (*grade*) ya wafanyabiashara. Mhe. Spika, kama ukiangalia katika jaduweli hili kama alivyosoma hapa Mhe. Naibu Waziri, kwamba tumejaribu kuweka mambo ambayo kamati imewafikiana na sisi kuweka jaduweli ambalo kwamba limeweka *grade* au uwezo wa mfanyabiashara.

Kwa kweli sisi tulikuwa na wazo kwamba hatutaki *discrimination* katika sheria na ilikuwa tunashughulika sana kosa na wala sio mtu. Lakini kwa kuridhika kutokana na maelezo tuliyopata, basi tumekubali na tumeweka katika grade hizo kama Mhe. Naibu Waziri alivyozizungumza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna suala moja la adhabu ya kifungo. Kwa kweli ningewaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wakubaliane na mimi masuala ya vifungo na biashara haziendi pamoja. Kwa mfano tukitaka biashara ishamiri Zanzibar na tukitaka kujenga uchumi wa kibiashara kama ilivyoasili ya Zanzibar, basi tujaribu kujiepusha na sheria za kuwafunga wafanyabiashara.

Jambo la msingi kwa wafanyabiashara watozwe faini walipe, wafanyabiashara wanyimwe leseni za kufanyabiashara, lakini wafanyabiashara wasifungwe na

tukiwafunga watakimbilia sehemu nyengine ambako hawafungwi na mambo ya kufungana fungana sasa tuyaondoshe. *(Makofi)*

Kwa mfano hapo Dubai kwa kweli hakuna hata kesi moja ya traffic ambayo mtu anapelekwa mahakamani, isipokuwa mtu anajua moja kwa moja nikipita *wrong site* faini yangu ni Dirham 300, niki-*park* pahala sipo faini yangu ni Dirham 300, nikifanya kosa la kwanza, la pili na la tatu basi leseni yangu ninanyang'anywa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, haya ndio masuala ya kuwasaidia kujenga misingi mizuri ya kibiashara, lakini tukiwa na sheria za kuwafunga wafanyabiashara basi tutaua biashara na ule msingi hasa wa sheria hii utakuwa umeporomoka moja kwa moja.

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba chonde chonde tuache kabisa katika Sheria ya Biashara kuzuia vipengele vya kufungana, isipokuwa tutie vipengele vya kutoza faini nztio tena kubwa na ina faida yake.

Vile vile, katika suala ambalo amelizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba fikra zake kuwa pale Katibu wa kamati atoke katika wizara lakini awe mwanasheria na yule Mkurugenzi awe mjumbe wa kudumu na mimi nakubaliana nalo moja kwa moja. Kwa hivyo, kifungu kile cha sheria nakikubali kibakie pale pale na wala hapo sina pingamizi na ninaamini kwamba italeta sura nzuri zaidi kwa mawazo yake Mhe. Mjumbe.

Pia, kuna sheria Nam. 50(3) kifungu mamlaka makubwa anayopewa waziri katika suala la kurekebisha hizi jaduweli ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza. Mhe. Spika, mimi sina hoja na hilo, isipokuwa tu naomba kifungo kiondolewe katika masuala ya biashara. Lakini kushauriana na kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mimi hili naliafiki moja kwa moja.

Mhe. Spika, kuhusu adhabu ya papo kwa papo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwenye kifungu cha 51(4) kwamba adhabu ya papo kwa papo italeta matatizo ya rushwa. Mhe. Spika, kwa hivi sasa katika dunia ya leo kama nilivyosema kwamba kesi nyingi ndogo ndogo zinakwenda katika adhabu za papo kwa papo, lakini adhabu hizi tayari zimeshaekewa kiwango. Kwa hivyo, anayepewa adhabu haonani na yule ambaye anamuadhibu.

Kanuni inasema kwamba aliyetenda kosa hili akikiri kama amefanya kosa lile basi analipa 50,000/= na ikiwa hakukiri atakwenda mahakamani. Lakini mimi nimesema kwamba jamani kweli nimetenda kosa na ninajua faini yake kosa hili ni

shilingi 100,000/= na niko tayari kulipa, basi anaruhusiwa alipe na kesi ile imekwisha.

Hali hiyo, inapunguza mrundiko wa kesi nyingi ndogo ndogo mahakamani ambapo tunatumia fedha nyingi za serikali. Kwa hivyo, utaratibu huu uko nchi nyingi sana umekuwa unatumika hasa kwa *experience* yangu mimi nchi ya Dubai, Abu Dhabi na Sharjah, yaani adhabu nyingi za Manispaa zinakuwa za hapo kwa papo.

Mhe. Spika, naomba suala hili Mhe. Mjumbe alifikirie zaidi kwamba ikiwa zile *fees* zitakuwa zimeelezwa wazi kila kosa katika Kanuni limeeleza nini adhabu yake, basi ninaamini kwamba itakuwa hakuna ile *loophole* ya mtu kutoa rushwa. Kwa hiyo, ninaomba suala hili Mhe. Mjumbe atusaidie kama anayo mawazo mengine, lakini nahisi itasaidia hizi kesi ndogo ndogo zinazojitokeza ambazo zinawasumbua wafanyabiashara na wafanyabiashara hawana muda ukiweza kuwafanyia hukumu zao haraka haraka ni bora.

Lakini mfanyabiashara leo anakwenda mahakamani miaka miwili kwa kesi ya kutozwa faini ya shilingi 100,000/=. Kwa maana hiyo, hii haileti mazingira mazuri kwa mfanyabiashara kwamba yeye kwa muda wa miaka miwili anakwenda mahakamani kwa kesi ya kutoa shilingi 100,000/= wakati yupo tayari alipe shilingi 100,000/= na kesi imalizike.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Mwakilishi aliangalie kwa undani zaidi na aone kwamba ipo haja ya kuona sheria ya papo kwa papo ipo, lakini lazima Kanuni ieleze wazi ile *amount* ya kila kosa.

Kuandaa Ripoti ya Mwaka Mhe. Spika, ni kweli kuna haja ya kutayarisha ripoti ya mwaka ya Biashara na kuitoa kwa jamii. Kwa hiyo, serikali inakubaliana na hoja hiyo moja kwa moja na imewekwa kama ni jukumu moja la Idara hii ya Biashara na kuongeza kifungu kipya Nam. 5(m).

Mhe. Spika, taaluma kwa wafanyabiashara wa mitaani (*Street Trading*) ni muhimu kwa mfanyabiashara yeyote kuwa na uelewa wa bidhaa anayouza au huduma anayoitoa, ili mtumiaji aweze kufahamishwa. Kwa mfano mfanyabiashara wa tungule anatakiwa kumueleza mnunuzi kwamba tungule hizi ni za leo au jana ama juzi.

Suala hili pia katika huduma Mhe. Spika, katika jimbo langu kuna mama mmoja amepata maradhi ya baridi akaitwa mganga kwenda kumfanyia dawa, yule mganga alipokwenda kumfanyia dawa, yule mama akamchua na mama yule akapiga kelele

sana maana yake mguu mmoja na mkono mmoja havifanyikazi, sasa yeye ule mguu mbovu ndio anaoung'ang'ania, akapiga kelele sana lakini hakusikilizwa na asubuhi kuamka mguu wote umevimba.

Sasa nilipokwenda kumuangalia mimi, akataka lazima niangalie mguu wake baada ya miezi mitatu, yaani mguu wote umekuwa kama rungu tu si mkuu tena, kumbe vile yule mganga mguu ameuvunja na ikabidi apelekwa Hospitali ya Mnazimmoja akatiwa pale la chuma na piopio baada ya kuwa yeye amepata maradhi ya baridi akawa mlemavu wa mara ya pili tena. Kwa hivyo, lazima watu wajue wanaofanyabiashara za huduma na zile biashara za bidhaa wajue athari zake pamoja na madhara yake.

Mhe. Spika, ninaye mtoto mwengine hivi sasa ambaye amekwenda kupimwa na sisi tulifikiri anayo Kesa ya Ini, baada ya kupimwa ameonekana kwenye ini lake hakuna madhara ya dawa za *chemicals*, lakini anayo madhara ya dawa za mitaani. Kutokana na hali hiyo, ni lazima mafunzo haya yapatikane kwa wafanyabiashara pamoja na wale wanaotoa huduma pia, kwamba wajue wanachokifanya sio wanasukuma wanavunja watu miguu, shingo na halafu ikawa mashaka mengine, hasa bidhaa za vipodozi.

Kwa mfano wengine wanajitia mafuta ya vipodozi kumbe yana madhara, tuliambiwa mafuta ya mabuyu yanaondoa *cholesterol* kumbe baadaye imeonekana mafuta ya ubuyu hayafai kabisa kwa matumizi ya binadamu. Kwa hiyo, elimu hii ni muhimu sana na wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine itafanyakazi za ziada kuona kwamba elimu hiyo inatowa.

Mhe. Spika, kuhusu Idara ya Biashara, kwa kweli hivi sasa Idara ya Biashara ipo na mkurugenzi yupo ambaye ameteuliwa na Mhe. Rais. Sheria hii inaipa idara hii majukumu ya kuweza kusimamia vyema shughuli za uendeshaji biashara hapa Zanzibar kama ilivyoelezwa katika kifungu 5 cha sheria hii. Utaratibu huu pia umetumika kwa Idara ya Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Nam. 12 ya mwaka 1996. Hoja hii imezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe akiwemo Mhe. Hamza Hassan Juma, ambapo hivi punde aliielezea.

Mswada kutozingatia sheria zilizofutwa. Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Biashara wa mwaka 2013 umezingatia vya kutosha mambo muhimu yaliyoelezwa katika sheria zinazopendekezwa kufutwa kama hivi ifuatavyo:-

1. Sheria ya Biashara Nam. 4 mwaka 1989 imeeleza uboreshaji wa Bodi ya Ushauri wa Biashara, kazi zake na kuanzisha utaratibu wa uendeshaji wa

bidhaa hizo. Mambo hayo yote yamezingatiwa vya kutosha katika Sheria mpya ya Biashara ya mwaka 2013 kama ilivyoelezwa katika sehemu ya tatu kifungu Nam. 6 mpaka Nam. 11, sehemu ya saba kifungu Nam. 38, 41 na 42 vya sheria hiyo.

2. Sheria ya Kuzuia Magendo ya Bidhaa Muhimu Nam. 5 ya mwaka 1986, imeeleza bidhaa muhimu zilizodhibitiwa na bidhaa zilizopigwa marufuku chini ya sheria hiyo. Mambo hayo yote yamezingatiwa kwa upana zaidi katika Sheria mpya ya Biashara ya mwaka 2013 kama ilivyoelezwa katika sehemu ya saba kuanzia kifungu cha 30 mpaka 38 na sehemu ya nane kifungu cha 39 mpaka 40 cha sheria hiyo mpya.

3. Kanuni za Sheria za Biashara za mwaka 1980 zimeeleza kuhusu utaratibu wa uuzaji wa bidhaa pamoja na wajibu wa mfanyabiashara. Mambo hayo yote yamezingatiwa vya kutosha katika Sheria mpya ya Biashara ya mwaka 2013 kama ilivyoelezwa kwa upana wake katika sehemu ya 6 kuanzia kifungu cha 20 mpaka 29 cha sheria hii inayopendekezwa.

Mhe. Spika, naomba isije katika uandishi wa kisheria hizi. Vile vile, katika sheria hii kumezuka suala la uandishi kuna maneno fulani fulani ambayo yanaleta utata basi tumeweza kuyarekebisha na mtayaona katika jaduweli hii yameelezwa wazi wazi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika kwa ufupi maelezo yote au mengi sana ambayo yametolewa na kamati ya Fedha, Biashara, na Kilimo, mawazo yote ambayo yametolewa na wachangiaji wetu tumeya-*accommodate* katika sheria hii kwa sababu tunajua kwamba mawazo hayo ni muhimu sana na yatasaidia sana kuweka sheria hii katika misingi bora.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba sheria hii hivi sasa imekuwa ni nzuri baada ya kupata mawazo yote hayo na ninawataka wajumbe wako wa Baraza lako tukufu wakubali marekebisho haya na kupitisha sheria hii, ili tukafanyekazi kwa pamoja.

Baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, ahasante sana. Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Biashara Zanzibar, 2013

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika
Kifungu 2 Eneo na Matumizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Idara ya Biashara

Kifungu 4 Kuanzishwa kwa Idara ya Kusimamia Biashara na Uteuzi wa Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5 Kazi za Idara pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tatu

Baraza la Ushauri

Kifungu 6 Kuanzishwa kwa Kamati
Kifungu 7 Muundo wa Kamati pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 Kazi za Kamati pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9 Mkutano wa Kamati pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 Fedha za Baraza
Kifungu 11 Taarifa ya Mwaka

Sehemu ya Nne

Mamlaka ya Usimamizi

Kifungu 12 Uwezo wa Usimamizi wa Jumla pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13 Uwezo wa Wasimamizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 Amri Kutoka kwa Wasimamizi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano

Usajili wa Biashara na Leseni

Kifungu 15 Usajili wa Biashara pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16 Utoaji Leseni za Biashara
Kifungu 17 Mipaka ya Mamlaka ya Leseni ya Biashara pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18 Maombi ya Usajili na Leseni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19 Kazi za Mamlaka ya Utoaji wa Leseni pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Uuzaji wa Baadhi ya Bidhaa na Utoaji Huduma

Kifungu 20 Uuzaji wa Baadhi ya Bidhaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 Wajibu wa Mfanyabiashara pamoja na marekebisho yake
Kifungu 22 Wajibu wa Waandaaji wa Biashara pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23 Wajibu wa Muuzaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24 Mahitaji katika Uuzaji wa Bidhaa na Utoaji wa Huduma pamoja na marekebisho yake
Kifungu 25

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake. Katika mchango wangu kwenye kifungu hichi nilieleza wasi wasi wangu kuhusu kifungu cha 25(3) hasa juu ya mgongano ambao unaojitokeza mara nyingi kati ya Serikali Kuu kupitia wizara na Serikali za Mitaa kupitia Manispaa na Halmashauri katika kusimamia masuala ya masharti ya

biashara hasa kwa mujibu kwa kifungu hichi kwamba biashara za mitaani na sokoni.

Sasa nilitoa indhari na katika majumuisho sikupata maelezo ya kuridhisha, basi ninaomba kidogo Mhe. Waziri anisaidie kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba nini ulikuwa msimamo wa wizara kuhusu hoja ambayo nilikuwa nimeitoa, ili nijiridhishe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ni kweli katika *item* hii sikutoa maelezo kwa ufasaha kwa ajili ya kuokoa muda. Lakini nasema kwamba Kanuni anatunga Waziri wa Biashara, taratibu atazipata kutoka katika hizo Manispaa pamoja na Halmashauri. Kwa hivyo, taratibu Mhe. Waziri anaweza akazikubali au akazikataa, hivyo taratibu si Kanuni, isipokuwa taratibu zikiwafikiana na Kanuni basi ahalani wasahalani na ikiwa hazikuwafikiana basi Kanuni zitatafautiana.

Kwa maana hiyo, taratibu viongozi tunawapa nafasi kwa sababu wao wana-*deal* na wale wafanyabiashara. Kwa hiyo, taratibu wakizipanga basi tutaziangalia na lazima taratibu zao ziende na Kanuni pamoja na sheria. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ufafanuzi huo wa Mhe. Waziri nimeridhika na ninaamini kwamba utasimamiwa katika utekelezaji. Kwa hivyo, naomba tuendelee.

Kifungu 25	Kufanya Biashara za Mtaaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 26	Ufanyaji Biashara Sokoni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27	Kufanya Biashara kwenye matokeo ya kijamii
Kifungu 28	Mambo ya Kuzingatia katika Utoaji wa Vibali vya Uuzaji
Kifungu 29	Punguzo la Bei la Bidhaa pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Saba

Udhibiti wa Uingizaji na Usafirishaji Bidhaa

Kifungu 30	Bidhaa zenye Kudhibitiwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 31	Ombi la Kutoa Kibali cha Uingizaji au Usafirishaji Bidhaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 32	Utoaji wa Kibali pamoja na marekebisho yake

Kifungu 33 Utoaji wa Kibali cha Uingizaji na Usafirishaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 34 Kufutwa kwa Kibali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 35 Uwezo wa Waziri wa Kupiga Marufuku au Kudhibiti Uingizaji au Usafirishaji wa Bidhaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 36 Utoaji wa Kibali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 37 Kupiga Marufuku kwa Usafirishaji wa Bidhaa bila ya Kibali cha Waziri
Kifungu 38 Utaratibu wa Kuingiza, Kusafirisha Bidhaa pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nane

Bidhaa Zilizozuiliwa na Zilizopigwa Marufuku

Kifungu 39 Bidhaa Zilizopigwa Marufuku na Kudhibitiwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 40 Bidhaa Zilizopigwa Marufuku na Kuzuiliwa Kusafirishwa
Kifungu 41 Uingizaji wa Mizigo kwa Usafirishaji
Kifungu 42 Uwezo wa Afisa wa Forodha pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tisa

Makosa na Adhabu

Kifungu 43 Kufanya Biashara Sehemu Isiyoruhusiwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 44 Makosa Yanayohusiana na Masharti ya Bidhaa na Huduma pamoja na marekebisho yake
Kifungu 45 Makosa Yanayohusiana na Uambatanishaji wa Nyaraka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 46 Kutokuwa na Kibali cha Uingizaji au Usafirishaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 47 Kutoa Taarifa za Uongo pamoja na marekebisho yake
Kifungu 48 Marufuku Kumpa Mtu Mwenye Kibali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 49 Uingizaji, Usafirishaji au Uhaulishaji wa Bidhaa Zilizopigwa Marufuku pamoja na marekebisho yake
Kifungu 50

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa wakati nilipokuwa nikichangia kifungu cha 50 nilizungumzia zaidi kifungu cha 50(3) ambacho kimeongezwa na kamati na baada ya maelezo ya Mhe. Waziri kwamba yeye hana tatizo, kwamba ile kazi ya kupitia jaduweli ifanywe *subject to* au kwa ridhaa ama kwa kuthibitishwa na kamati inayohusika na hilo sina tatizo nalo. Kwa hivyo, hilo ninamshukuru kwanza na naamini litazingatiwa katika kufanya marekebisho ya mswada.

Lakini kidogo nimepata matatizo katika maelezo yake ya majumuisho Mhe. Waziri na nimeomba ufafanuzi hapa Mhe. Mwenyekiti, ili tukipitisha tujue tumepitisha nini. Mhe. Mwenyekiti, mswada ulivyoletwa mwanzo ulikuwa unajumuisha faini na vifungo na huu ni mswada ambao umeletwa na serikali chini ya Waziri.

Baadaye kamati pamoja na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali walipotahadharisha na hasa kwa muongozo mzuri wa Mwenyekiti wa Kamati, basi wakapendekeza masuala haya yawekwe katika jaduwali na jaduwali la 4 ambalo limeambatanishwa kwenye waraka ule wa marekebisho ambalo limewekwa chini ya kifungu cha 50(2). Kwa hiyo, kifungu chake ni hichi umetaja bado faini na vifungo.

Lakini Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho ametuomba kwamba Wajumbe wa Baraza tena ni hoja makini sana kwamba katika kuweka mazingira mazuri ya biashara katika dunia ya leo, basi masuala haya huwa hayana adhabu za vifungo na badala yake kunakuwa na adhabu ya faini hata kama ni kubwa kiasi gani. Mhe. Mwenyekiti, sasa napata matatizo kidogo kwa sababu kiilivyo tumechukulia kama maelezo ya Waziri ya majumuisho ndio tunayoyapitisha.

Kwa hivyo, nataka maelekezo yako Mhe. Mwenyekiti na kiti chako kwamba je, kwa maelezo yale ya Mhe. Waziri tunafuta ile *colum* yenyewe vifungo katika jaduweli lililokuwa limetajwa hapa kama jaduweli Nam. 4 na badala yake tunaweka adhabu ya faini tu kwa sababu haya yalikuwa ndio maelezo ya Mhe. Waziri ambayo ndiyo yanayochukuliwa kwamba ni maelezo ya msingi katika kupitisha mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelekezo ya kiti au Mhe. Waziri, ili tujue tunapitisha nini Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na pia ninamshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwa hivyo, mimi ninaomba suala la kifungo tulirekebishe katika sheria hii, ili biashara iweze kuimarika na kuzidi katika nchi yetu na biashara za siku hizi basi suala la kifungo liondoke na

ndio maana hili ni ombi nimelileta kwenu kwa ajili ya kulitafakari na kuliangalia Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imekubali kwamba hapa chini kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja. Lakini ninaomba suala la kifungo katika sheria hii lisiwepo kabisa na hilo ndilo ombi langu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mjumbe mimi ambaye jimbo langu linaongoza kwa shughuli za biashara sina tatizo na pendekezo la Mhe. Waziri. Lakini nafikiri sasa sijui tutafanya utaratibu gani na mimi nakubali pendekezo la Mhe. Waziri na ningewaomba wenzangu kwamba tukubali kwa maana hiyo basi kwenye *colum* ya kifungo katika jaduweli Nam. 4 iondoshwe na ibakie na faini kwa ajili ya kumridhia Mhe. Waziri, kwa sababu pendekezo lake ni la msingi.

Kwa hivyo, kama ingelikuwa kuna makosa mengine makubwa zaidi basi ningekubali kwamba bado kunahitajika kifungo, lakini nadhani haya yanakuwa-*covered* katika sheria nyengine mbali mbali na kwa mimi binafsi sina tatizo, basi nadhani tungeomba kiti chako kitusaidie utatuhoji vipi Mhe. Mwenyekiti katika kupitisha kifungu hichi sifahamu pamoja na marekebisho yake kwa maana hayo aliyotoa Mhe. Waziri na wala mimi sina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nafikiri ni sawa unachokisema kwamba sasa marekebisho mengine ni ile kuondoa vifungo kwenye ile jaduweli. Tunaendelea.

Kifungu 50	Adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 51	Adhabu za papo hapo pamoja na marekebisho yake
Kifungu 52	Makosa Yanayofanywa na Makampuni na Mashirika
Kifungu 53	Vifaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 54	Uwezo wa Kutunga Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 55	Kufuta na Kubakiza pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu hadi kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali na naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Biashara Zanzibar, 2013

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Biashara ya Zanzibar, 2013 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kuwashukuru kwamba shughuli ambazo zimepangwa kwa leo zote zimemalizika, kutokana na mashirikiano makubwa ambayo Waheshimiwa Wajumbe mumeyatoa, ili kumaliza shughuli hizi.

Baada ya hayo, sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 18/10/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:30 Kikao kiliakhirishwa hadi tarehe
18/10/2013 saa 3:00 za asubuhi)